



UKURASA 22

**WAZIRI** Ulega atema cheche TANROADS

UKURASA 4

**WAAJIRIWA** wapya serikalini kupimwa utimamu wa akili

UKURASA 2

**SERIKALI** yajivunia mavuno uwekezaji wa bandarini Dar

UKURASA 5

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Ijumaa Desemba 20, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581896
epaper.ippmedia.com
LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashedigital

## KUNG'ATWA NA NYOKA...

# Kifo cha mama kituo cha afya chazua kasheshe

**WATUMISHI** watatu tayari kikaangoni... *Ukurasa wa 2*



## Mwinyi afurahia Dola kuanguka, neema tele kwa wananchi wake

UKURASA 3

## Kada mwingine wa CHADEMA ajitosa kuwania kiti cha Mbowe

**Na Elizabeth Zaya**

MBIO za kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) zimezidi kunoga baada ya jana mwanachama mwingine kujitosa kuwania nafasi hiyo.

Mwanachama huyo kutoka tawi la Kunduchi Mtongani, Dar es Salaam ni Romanus Mapunda. Alifika katika ofisi za makao makuu ya chama hicho jana mchana kuchukua fomu. Romanus anafanya idadi ya wanachama waliochukua fomu ya kuwania

**Endelea** Uk. 2

## JK asimulia misukosuko aliyopitia Msajili Tendwa

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitoa heshima za mwisho kwa marehemu John Tendwa, Msajili Mstaafu wa Vyama vya Siasa, alipomwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika maombolezo na kuaga mwili wa marehemu Tendwa kwenye viwanja vya Karimjee jijini Dar es salaam jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

**MICHEZO** **KAMERA MPYA 200 UWANJA WA MKAPA** UK. 24 **KATUNI** UK. 6

HABARI KITAIFA

# Wasimamishwa kazi madai kifo mama aliyeng'atwa na nyoka kukosa matibabu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SAKATA la mgonjwa Juliana Obedi (43) aliyeng'atwa na nyoka kufia katika Kituo cha Afya cha Magugu, Babati mkoani Manyara, limewang'oa kwenye ajira watu watatu wanaodaiwa kumcheleweshea matibabu kwa saa sita, wakitaka kulipwa kwanza Sh. 150,000.

Tayari serikali imetangaza kuanza uchunguzi kuhusiana na tukio hilo kwa ushirikiano wa timu ya wataalam wa halmashauri, mkoa na mabaraza ya kitaaluma.

Taarifa iliyotolewa kwa umma jana na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Benedict Ntabagi, iliwataja waliosimamishwa kazi kupisha uchunguzi ni watoa huduma watatu wa Kituo cha Afya Magugu, ambao ni ofisa tabibu, ofisa muuguzi msaidizi na mteknolojia wa dawa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya Desemba 18, mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji amefikia uamuzi huo ili kupisha uchunguzi wa tukio hilo kutokana na watumishi hao kutuhumiwa kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

"Pamoja na changamoto iliyojitokeza ya mgonjwa huyo kucheleweshwa huduma katika kituo cha afya kwa saa sita baada ya kung'atwa na nyoka, mkono wa kulia aliong'atwa ukiwa umevimba na kubadilika rangi, vinaashiria tayari sumu ilikuwa imemwathiri sana mama huyo," ilieleza taarifa hiyo.

Vilevile, taarifa ilieleza kuwa wataalamu hao wa afya, walipaswa kumpatia huduma stahiki zote kwanza mgonjwa kwa dharura na masuala ya malipo yangekamilishwa baadaye.

Taarifa hiyo ilieleza zaidi kwamba kwa mujibu wa Sera ya Afya ya Mwaka 2007 na miongozo yake makundi maalumu yakiwamo ya wajawazito, watoto chini ya miaka mitano na wazee wasiojiweza wanatakiwa kupatiwa matibabu bure.

Aidha, zinapohitajika huduma za dharura, mgonjwa anatakiwa kuhudumiwa na kama hayumo kwenye kundi la msamaha, basi taratibu za malipo zifuate baada ya kukamilisha huduma.

Kwa muktadha huo, taarifa ilisema uchunguzi wa tukio hilo unaendelea kufanyika kwa ushirikiano wa timu ya wataalamu wa halmashauri, mkoa na mabaraza ya kitaaluma na hatua zitachukuliwa kwa wote watakaobainika kuwa na hatia katika tukio hilo.

Pia taarifa ilisema halmashauri inaendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya na kuitaka jamii mara wanapopata dharura ya kiafya zinazohitaji matibabu ya haraka kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma mapema bila kuchelewa.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Wauzaji wa chenji za sarafu wakiwa kazini kwenye kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mwingine ajitosa kuwania uenyekiti CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

MBIO za kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) zimezidi kunoga baada ya jana mwanachama mwingine kujitosa kuwania nafasi hiyo.

Mwanachama huyo kutoka tawi la Kunduchi Mtongani, Dar es Salaam ni Romanus Mapunda. Alifika katika ofisi za makao makuu ya chama hicho jana mchana kuchukua fomu.

Romanus anafanya idadi ya wanachama waliochukua fomu ya kuwania nafasi hiyo kuwa wawili baada ya Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara, Tundu Lissu kuchukua na kurejesha.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuchukua fomu, Romanus alitamba ataleta ushindani katika uchaguzi huo. Ana uhakika wa kushinda kwa sababu ana kundi kubwa la watu wanaomuunga mkono.

"Nimeamua rasmi kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya uenyekiti wa CHADEMA, nina sababu nyingi sana zilizonisukuma. Nimeona nina sifa ya kuwa mwenyekiti wa chama hiki na nina wadau wa kutosha na kuniunga mkono na ninaamini nitashinda, wadau wamenichangia fomu na kesho (leo), nitarudisha fomu," alisema.

Akichaguliwa kukalia kiti hicho, atafanya makubwa ikiwamo kuweka mikakati mizuri ya chama hicho kushika dola katika Uchaguzi Mkuu ujao.

"Ninachowaahidi wanachama wa CHADEMA, kwanza waniamini. Pili, mimi ni mtu wa kuamsha popo, wajenge imani na mimi twende pamoja, mwaka 2025 tunakwenda kushinda uchaguzi na tunachukua nchi mapema kabisa," alisema.

Aliongeza: "Sisi tunategemea kushinda serikali, lakini hatuwezi kukitoa Chama Cha Mapinduzi (CCM) madarakani kwa kuhubiri, tunatakiwa tukakitoe madarakani kwa kupiga kura."

Mwenyekiti Taifa wa chama hicho, Freeman Mbowe hajaweka wazi kama atagombea au la, anatarajia kutoa uamuzi wake kesho atakapozungumza na wahariri wa vyombo vya habari.

Juzi akizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake Mikocheni, Dar es Salaam, Mbowe alisema maombi yao kumshawishi atetee tena nafasi yake ameyapokea, lakini atafanya uamuzi baada ya saa 48.

Mbali na nafasi ya uenyekiti wa chama, nafasi zingine zinazogombaniwa ni Makamu Mwenyekiti Bara na Makamu Mwenyekiti Zanzibar.

Nyingine ni Katibu Mkuu Baraza la Wazee (BAZECHA) Bara, Naibu Katibu Mkuu Bara, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar na Mweka Hazina.

Zingine ni wajumbe watano wa baraza kuu ambao wanne ni kutoka Tanzania Bara na mmoja ni kutoka Zanzibar pamoja na wajumbe 20. Kati yao, 15 ni kutoka Tanzania Bara na watano kutoka Zanzibar.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Waajiriwa wapya kupimwa utimamu akili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI kupitia Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, inatarajia kuanza kuwapima utimamu wa akili (psychonomic test) waajiriwa wapya ili kuona afya zao za akili kabla ya kuanza kutumikia nafasi zao.

Aidha, serikali imekemea utovu wa nidhamu, rushwa,vitisho na ubabe kwa waajiri na watumishi wa umma huku ikisema kuna dereva kwenye halmashauri amenyimwa gari kisa hakugawana posho ya kujikimu na bosi wake.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, aliyasema hayo jana alipokuwa akifunga kikao kazi cha siku tatu cha wakuu wa idara za rasilimali watu na utawala katika utumishi wa umma kutoka kwenye wizara, wakala, mamlaka, mashirika na taasisi za serikali.

Alisema mwajiriwa mpya anaweza kuwa amekidhi vigezo vya kitaaluma na kielimu lakini kisaikolojia akawa na shida, hivyo ni muhimu kuangalia afya ya akili.

"Sekretarieti ya ajira wamekuja na utaratibu wa kuwafanyia upekuzi waajiriwa wapya 'psychonomic test' ili kujua mtu tunayempeleka kama kuna shida fulani, tufanyie marekebisho ili akiingia atusaidie kazi vizuri.

"Kuna halmashauri nilikwenda nikakuta kijana mwaka wa nne hataki kupangiwa kazi yoyote, muda wote ni kuwatisha waajiri pale na bosi wake wanayefanya naye kazi wanavutana mashati wana kesi hadi polisi.

Yaani ajira mpya halafu mbabe nikawaambia mnawezaje kuishi? Tumewapa mamlaka hamtaki kutumia nikasema sasa nitawasaidia namna ya kufanya kazi kwenye utumishi wa umma,"alisema.

Alisema vijana wanaoingia kwenye utumishi wa umma wanadhani wanakwenda kufanya utovu wa nidhamu na kujiingiza kwenye mikopo ambayo inachangia washindwe kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

"Vijana wetu wanaingia kwenye utumishi wa umma wanajiingiza kwenye mikopo ambayo mwisho wa siku wanakosa utulivu wa kufanya kazi, lazima tuwape elimu ya fedha kwa kuwa anaweza kuingia kazini akadhani anafanya kazi bure kumbe mshahara wake ameutumia vibaya kwenye mikopo huko ya kausha damu,"alisema.

Sangu aliwahimiza maofisa utumishi kuwaangalia vijana hao ili kuwa na watumishi wenye tija kwa kuwa utumishi wa umma una utamaduni wake na kwamba kumekuwapo na kasumba wanapofika waajiriwa hao hakuna mafunzo, maelekezo, miiko na wengine wanaangukia kwenye vitendo vibaya.

Kuhusu uhamisho, Sangu alisema maombi 14,000 yako kwa waajiri hayajafanyiwa kazi na moja la ni maofisa utumishi kutotaka kufanya uamuzi hali inayowakatisha tamaa watumishi na kukosekana kwa utulivu mahali pa kazi.

"Tufanyie maboresho ya mfumo wa uhamisho kwa kuwa kuna waajiri hawawajibiki na wanachukua muda mrefu kutokushughulikia uhamisho, ili linapofika ombi halijafanyiwa kazi siku saba lihame moja kwa moja ngazi nyingine na likifika kwa Katibu Mkuu bila maoni yako utawajibishwa mhusika,"alisema.

Aliwataka wakafanye mipango kwenye bajeti zao wahakikishe wanatenga fedha za uhamisho.

"Malimbikizo ya mishahara huko kwenye halmashauri kwa mfano kuna mtumishi anadai zaidi ya miaka 10 na deni lake ni zaidi ya Sh. milioni 60 na kisingizio kinachotolewa ni madai yako Utumishi wanachelewesha jambo ambalo si kweli, "alisema.

Katika hatua nyingine, alikemea tabia ya maofisa utumishi kuwafukuza kazi watumishi kwa kuwaonea na kwamba kwa mwaka huu wa fedha zaidi ya mashauri 300 yamerudishwa yakaanze upya na yanaisababishia serikali hasara.

Kuhusu rushwa, alisema kuna waajiri wanachukua rushwa ndio watoe huduma kwa watumishi huku akidai kuwa kuna halmashauri imepokea karatasi za wadada zaidi ya 30 wanamtuhumu mtu mmoja kwa rushwa ya ngono na tayari ameagiza Takukuru ifanye uchunguzi.

Awali, Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Juma Mkomi alisema miezi minne iliyopita kuna mtumishi aliandika barua kuwatuhumu na bosi wake kwa sababu tu ya uhamisho, hajafukuzwa kazi, hajapoteza cheo na hajafanyia jambo lolote. "Tunajiuliza huyu mtumishi akili yake ipo timamu anayofanya huku nyuma hayakubainika wakati anaajiriwa? Tumesisitizana lazima mtumishi yeyote anayeajiriwa lazima vipimo vifanyike," alisema.

Alisema mtumishi huyo ana miaka minne kwenye utumishi lakini ameonesha tabia za hatari.

**HABARI KITAIFA**

# Dk. Mwinyi: Kushuka dola kutapunguza gharama za maisha

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kushuka kwa thamani ya dola nchini ni faraja kubwa kwa uchumi, kwa kuwa kutapunguza gharama za maisha kwa wananchi.

Aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar, wakati akizungumza na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba, pamoja na ujumbe alioongozana nao waliofika kumtembelea.

Rais Mwinyi alisema ni matarajio yake kwamba kushuka kwa dola kutasaidia pia, kupungua gharama za baadhi ya mahitaji katika maisha ikiwamo kupungua bei kwa bidhaa muhimu kama vile chakula na mafuta.

Alisisitiza kwamba bidhaa zote zilizoathirika kutokana na kupanda kwa dola duniani ni matarajio yake kwamba, zitarejea katika uhalisia wake.

Akizungumzia suala la uingizwaji wa bidhaa nyingi na athari za kupanda kwa dola, Rais Mwinyi alisema, iliathiri uchumi wa nchi licha ya kuwa baadhi ya bidhaa zinazozalishwa nchini zilifidia hasara hasa wakati wa mavuno.

Alitoa mfano wa bidhaa za chakula ikiwamo mchele na kusema kwa kiasi ilipunguza kasi ya uagiziaji kutoka nje.

Rais Mwinyi aliipongeza BoT kwa weledi wa kuendelea kuwahamasisha wananchi kuhusu kubadilisha noti za zamani zinazoondoshwa katika mzunguko kwa matumizi yao ya kila siku.

Aliahidi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendeleza ushirikiano na benki hiyo, ili kushajihisha jamii na kuwajengea uelewa wananchi wa kubadili noti za zamani kusaidia kuondoka katika mzunguko kwa wakati.

Gavana BoT, Tutuba alimweleza Rais Mwinyi kwamba, benki hiyo inaendeleza na mchakato wa kuondoa katika mzunguko noti za zamani za shilingi 20, 200, 500, 1000, 2000, 5000 na 10,000, kwa matoleo ya mwaka 1985 hadi 2003.

Alisema BoT imetoa muda maalumu kwa Watanzania kuanzia mwezi Januari, 2025 hadi Aprili, 2025, kuutumia muda huo kubadilisha noti za zamani kupitia ofisi zote za Benki Kuu ya Tanzania na benki zote za biashara kwa kupatiwa malipo yenye thamani sawasawa na kiasi kinachobadilishwa.

Gavana Tutuba alitoa rai kwa wananchi wenye noti za zamani kuzibadilisha au kuziweka amana kwenye benki yoyote ndani ya kipindi kilichowekwa.

Akizungumzia kushuka kwa thamani ya dola nchini, Gavana Tutuba, alisema ni hatua moja ya benki hiyo kuipandisha thamani na kuirejesha katika mzungungo wa soko, fedha ya ndani ambayo kwa kipindi kirefu ilishuka.

Alisema ametoa indhari kwa wafanyabiashara wote nchini pamoja na kuwajulisha Watanzania kwamba ni marufuku kwa mfanyabiashara yeyote kuuza ama kununua bidhaa kwa kutumia dola ama fedha yoyote ya kigeni.

Alisema kufanya hivyo ni kulitangaza na kulipandisha thamani soko la nje na kuua la ndani suala ambalo halikubaliki kisheria kwa mujibu wa sera na kanuni za soko na uchumi wa nchi.

Gavana Tutuba aliwashauri wafanyabiashara kote nchini wakiwamo wamiliki wa hoteli na sekta nyingine za utalii na uwekezaji, kuwashajihisha wateja wao kuendelea kufanya malipo kwa kutumia thamani ya fedha za ndani.

Kadhalika, aliwashauri pia kuweka mazingira ya kubadilisha fedha za kigeni katika sehemu zao za biashara ili wageni waendelee kutumia thamani ya fedha ya ndani.

Gavana Tutuba alisema matarajio yake kwa wafanyabiashara ni kupunguza bei ya bidhaa zao kutokana na kushuka kwa thamani ya dola, akizisihi mamlaka za serikali kuingilia kati ili kuwasaidia wananchi kupunguza mzigo wa gharama za maisha.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



**KUMRADHI:**
Katika gazeti letu la Desemba 18 tulichapisha picha hii ikiwa na makosa ya jina la Mkuu wa Majeshi nchini. Usahihi wa maelezo ya picha hiyo ni: Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha (kulia) akisalimiana na Mkuu wa Majeshi Jenerali Jacob Mkunda nje ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo wakati Jenerali Mkunda alipokwenda kujadiliana mambo mbalimbali ya kikazi.

# JK afichua yaliyomkuta Tendwa akitekeleza wajibu

**Na Halfani Chusi**

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, amefichua masahibu aliyoyapata aliyekuwa Msajili wa Vyama vya Siasa, John Tendwa, alipokuwa akitekeleza wajibu wake.

Wakati Kikwete akiibua hayo, Wiziri Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania kuendelea kumwombea Tendwa na kusema alikuwa kiongozi wa mfano wa kuigwa.

Akizungumza jana wakati wa ibada ya kuaga mwili wa Tendwa, aliyefariki mapema wiki hii katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) katika viwanja vya Karimjee, Dar es Salaam, Kikwete alisema wakati akitekeleza majukumu yake, aliwahi kufungiwa ndani ya ofisi za chama cha CUF Zanzibar, alipokwenda kufanya uhakiki lakini alisimamia msimamo wake.

Kikwete alisema Tendwa alikuwa na mchango mkubwa katika kujenga demokrasia ya vyama vingi katika nchi na kwamba haiwezekani kuzungumzia ustawi wake bila kulitaja jina lake.

Alisema alipigiwa simu na mmoja wa mtoto wa Tendwa kumjuza kwamba baba yake anaumwa na muda wote alikuwa anamtaja.

"Nikasema ninashukuru nikamuuliza hali yake inaendeleaje? Akasema hali yake ni ngumu yuko chumba cha uangalizi maalumu (ICU). Niliahidi kwamba nitatafuta nafasi nikamwone lakini nikawa nina safari, niliporejea nikasema ngoja nikamwone lakini nikapata taarifa ameshafariki.

"Msiba huu si wa familia tu ni wa kwetu sote. Niwape faraja familia ya mfiwa hamko peke yenu. Tendwa nimefanya naye kazi. Aliteuliwa mwaka 2001 mimi niliingia madarakani mwaka 2005 mwishoni na alimaliza kipindi chake 2013 baadaye nikamteua Jaji Francis Mutungi. Ninachoweza kusema alikuwa na sifa ya kusema ukweli," alisema.

Akizungumza katika hafla hiyo, Majaliwa alisema: "Nimekuja hapa kutoa salamu za pole za Rais Samia Suluhu Hassan na za kwangu. Tendwa alikuwa mtumishi wa umma katika ofisi mbalimbal na alikuwa mtumishi mwaminifu.

"Amefanya kazi yake vizuri sana katika vyama vya siasa hasa katika kipindi ambacho vyama vilikuwa vinajijenga."

Majaliwa alisisitiza taifa limepata pigo kubwa na kwamba jukumu lililopo kwa sasa ni kuungana na wanafamilia kuenzi mazuri aliyoyafanya katika utumishi wake.

**MUTUNGI AMLILIA**

Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, alisema Tendwa alikuwa mwalimu wake katika mambo mengi, ikizingatiwa kwamba alipokea kijiti cha uongozi kutoka kwake na yuko kwenye nafasi hiyo mpaka sasa.

Alisema Tendwa alijitolea kuhakikisha msingi wa demokrasi unajengwa ipasavyo na alikuwa mweledi katika kipindi chake. Pia alisema Tendwa alihakikisha ofisi inakuwa kiunganishi kwa vyama vya siasa.

"Mchango wake uliimarisha mazingira ya kisiasa amani na mshikamano vilitawala katika uongozi wake. Hatuwezi kuzungumzia mfumo wa vyama vingi bila kulitaja jina lake" alisema Mutungi

**ACT WAZALENDO**

Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Dorothy Semu alisema wataendelea kumkumbuka Tendwa kama kiongozi aliyesimamia vyama kwa uadilifu mkubwa.

"Tutamkumbuka kama kiongozi mlezi aliyesiamamia vyama kwa uadilifu na weledi mkubwa, kiongozi aliyesimamaia demokrasia ndani ya vyama na nje. "Kumuenzi Tendwa ni sisi viongozi kuendelea kuyasimamia aliyoacha na kuvikuza vyama siasa na demokrasia ya kweli" alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, Juma Ally Khatibu, alisema Tendwa alikuwa nguzo ya mazungumzo ya kitaifa na mshikamano wa kisiasa kwa kuwa aliongoza kwa hekima na kujenga mazingira ya siasa yenye heshima, usawa, na mshikamano baina ya vyama vya siasa.

"Katika nafasi yake kama Msajili wa Vyama vya Siasa, Tendwa alitoa mchango mkubwa katika kuimarisha misingi ya demokrasia ya vyama vingi. Alisimamia taratibu za vyama kwa haki na bila upendeleo, akijenga imani kati ya wadau wa siasa na wananchi," alisema. Viongozi Wengine walioshiriki kuaga mwili wa Tendwa ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Ummy Nderiananga, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Dk. Jim Yonaz.

Kwa mujibu wa ratiba ya msiba huo iliyotolewa na familia juzi inaonesha Tendwa anazikwa leo katika makaburi ya Ununio kwa Kondo Dar es Salaam.

# Mwili wa Ulomi waagwa, familia yatoa neno

**Na Mwandishi Wetu**

MWILI wa mfanyabiashara Daislei Ulomi aliyefariki dunia kwa ajali, uliagwa jana katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Madale Betheli, huku familia ikisema ni mipango ya Mungu.

Ulomi alipotea katika mazingira ya kutatanisha Desemba 11, mwaka huu na kuleta taharuki kwa ndugu jamaa na marafiki na Desemba 16, mwili wake ulipatikana katika Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala, Dar es Salaam.

Safari ya mazishi ya Ulomi ilianza jana saa tano asubuhi mwili wake ulipoondolewa kutoka katika hospitali hiyo na kupelekwa nyumbani kwao, Mikocheni kwa ajili ya sala fupi na baadaye ndugu, jamaa na marafiki kuaga.

Saa 7:00 mchana, mwili wa marehemu ulipelekwa kanisa KKKT Usharika wa Madale Betheli kwa ajili ya ibada ya mazishi.

Akitoa salamu za familia, kaka wa marehemu, Mrakibu Msaidizi (ASP) Elisante Ulomi, alisema kifo cha mdogo wake kilikuwa cha ghafla lakini ni mipango ya Mungu.

Alisema mdogo wake amewaacha katika wakati ambao bado walikuwa wanamtegemea lakini wanamshukuru Mungu kwa maisha yake hapa duniani

Alisema Ulomi alifariki dunia akiwa na miaka 43, wakati mkewe, watoto na familia wakiwa bado wanamhitaji lakini yote ni mapenzi ya Mungu na familia itaendelea kumwombea.

Pia alilishukuru Jeshi la Polisi kwa ushirikiano mkubwa lililouonesha kwa familia tangu kupotea kwa ndugu yao mpaka walipoupata mwili wake.

Aidha aliwashukuru jamaa na marafiki na KKKT kwa kuwashika mkono katika kipindi hicho kigumu wanachopita kama familia.

Mchungaji Kiongozi wa Usharika huo, Ruth Mdoe, alisema Ulomi alikuwa msharika mzuri wa kanisa hilo na alikubali kuongozwa kiroho na viongozi wa dini.

Alisema alishirikiana na kila mtu na bila kujali vipato vyao na kuwasihi waumini wa kanisa hilo kuiga hilo kama mfano kama huo kwa kuwa ndiyo msingi bora wa maisha.

Mchungaji Mdoe aliisihi familia ya marehemu kuendelea kuwa imara katika kipindi hiki akisema safari ya mpendwa wao ilikuwa imefikia mwisho kama itakavyokuwa kwa kila mwanadamu.

Akisoma wasifu wake, ndugu wa marehemu, Ennocent Munuo, alisema Ulomi alizaliwa mwaka 1981 na alikuwa askari polisi tangu mwaka 2006 mpaka umauti unamfika.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, Desemba 17, mwaka huu, alisema kuwa Ulomi alipata ajali Desemba 11, mwaka huu, maeneo ya Ubungo External na alipelekwa katika Kituo cha Afya Makuburi kisha mwili wake kuhifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala.



Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega, akizungumza na menejimenti ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) katika kikao kazi kilichofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Ulega atema cheche TANROADS

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega, ameagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kufanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha miradi ya dharura iliyo chini yake.

Waziri Ulega ametoa maagizo hayo kwenye mkutano wake na menejimenti na mameneja wa TANROADS wa mikoa yote nchini uliofanyika jijini Dodoma. Alisisitiza kuwa miradi ya dharura inapaswa kushughulikiwa kidharura.

"Fanyeni kazi kwa kasi tena usiku na mchana hususan kwenye miradi ya dharura ili kuwawezesha Watanzania kuondokana na adha ya miundombinu iliyoharibiwa", alisema.

Ulega aliwaambia mameneja hao kuwa wanatakiwa kuendana na kasi inayofanana na viwango vinavyoonekana wakati Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) linapopewa majukumu ya utekelezaji na serikali kwa sababu kuna mvua zinakuja na zinaweza kufanya maeneo yaliyoharibika kuharibika zaidi.

Alisema barabara zilizoharibika kwa sababu ya mvua ya masika iliyochanganyika na zile za El Nino zimesababisha usumbufu na kusimamisha shughuli za Uchumi, hivyo ni muhimu zikashughulikiwa kwa haraka. Mkutano wa Dodoma ulikuwa wa kwanza kwa Ulega kukutana na viongozi wa TANROADS tangu ateuliwe kushika wadhifa huo na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni.

Waziri Ulega pia alitumia nafasi hiyo kupongeza wafanyakazi wa wakala huo kwa kufanya kazi kwa bidii na weledi na katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, imekamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa zaidi ya kilometa 1,198 kwa kiwango cha lami.

Ulega ambaye pia ni Mbunge wa Mkuranga, aliwataka mameneja hao kufanya kazi kwa kujiamini na weledi mkubwa ili kuleta tija na ufanisi katika sekta ya ujenzi nchini ili kuondoa kero ya miundombinu mibovu kwa wananchi ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi.

Aidha, Ulega alitoa rai kwa mameneja wa mikoa yote nchini kuhakikisha maeneo yote yenye msongamano wa magari hususani kwenye majiji na manispaa yanafanyiwa usanifu yakinifu kwa ufasaha kulingana na mahitaji ya sasa na miaka mingi ijayo na kuratibiwa vizuri ili kupunguza tatizo hilo hatimaye kuwawezesha wananchi kufanya kazi zao kwa wakati.

Waziri Ulega aliwahakikishia mameneja hao kuwa serikali itaendelea kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali za makandarasi ili kuhakikisha wanafanya kazi kwa kasi ili kuendana na malengo ya serikali.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Balozi Mhandisi Aisha Amour, alisema TANROADS itaendelea kuhakikisha barabara kuu, za mikoa na madaraja yanajengwa ili kupitika wakati wote wa mwaka. Balozi Amour aliwataka mameneja wa TANROADS kuboresha usimamizi wa miradi, kulinda hifadhi za barabara pamoja na kupendezesha miji kwa taa za barabarani na utunzaji wa mazingira pembezoni mwa barabara.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# DC aongoza mamia kuaga miili askari wawili waliouawa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Mpwapwa, Sophia Kizigo, ameongoza mamia ya wakazi wa wilaya hiyo kuaga miili ya askari wawili wa Jeshi la Polisi waliouawa kwenye majibizano ya risasi wakati wakitekeleza majukumu yao.

Akiongoza tukio hilo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, Sophia alisema serikali imepokea kwa masikitiko makubwa vifo vya wapiganaji hao waliopoteza maisha wakiwa wanatekeleza majukumu yao.

"Serikali imepokea kwa masikitiko makubwa sana vifo vya askari hawa ambao wamepoteza maisha yao wakiwa wanatekeleza majukumu yao ya kila siku. Lakini niwashukuru raia kwa namna ambavyo mmetukimbilia kwani hakuna siku ambayo nimepokea simu nyingi sana na meseji kama ilivyo kuwa jana na leo," alisema.

Aliongeza: "Niwahakikishie kuwa serikali pamoja na wananchi tuko pamoja na Jeshi la Polisi katika kipindi hiki cha majonzi haya. Vijana hawa nilikuwa nawafahamu kutokana na kazi yangu kama tungekuwa tumeenda vitani ningesema wamefia vitani".

Aidha, alisema askari hao walikuwa wanapeleleza tukio la mkazi mmoja wa Mpwapwa ambaye aliporwa fedha na kwa bahati mbaya wakakutwa na kadhia hiyo.

"Mtu huyo aliporwa fedha zake na kujeruhiwa ndipo polisi walipata taarifa na kufanya upelelezi, ili upate uhakika ni lazima ufanye upelelezi, hivyo polisi walifanya upelelezi na kubaini wapi alipo huyo mtuhumiwa ama mshukiwa ili wamkamate na kumpeleka kwenye vyombo vya sheria. Lakini kwa bahati mbaya sana walipofika pale yakatokea majibizano wenzetu wawili hawa wakapoteza maisha yao," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, alisema majira ya saa saba usiku mtuhumiwa Atanasio Malenda (30) alidaiwa kumpora Yohana Lameck fedha kiasi cha Sh. milioni mbili kwa kutumia silaha.

Aliwataja askari waliofariki kwenye tukio hilo kuwa ni Jairo Kalanda na Alfred John, huku mtuhumiwa Atanasio akifariki alipokuwa akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa.

Alifafanua kuwa Askari hao wakiwa na wenzao walipata taarifa kuwa mtuhumiwa huyo aliyekuwa anatafutwa yupo nyumbani kwake Msagali.

**HABARI KITAIFA**

# Serikali yajivunia mavuno uwekezaji wa DP World




Msemaji Mkuu wa Serikali ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana wakati alipokuwa akitolea ufafanuzi miradi ya Serikali kuendelea kufanyiwa kazi ili kuwaondolea kero wananchi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema uwekezaji wa kampuni ya DP World bandarini "unalipa", ikijivunia kuongezeka ufanisi katika uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa alitangaza neema hiyo alipozungumza na waandishi wa habari kwenye Ukumbi wa Mamlaka ya Bandari (TPA) jijini Dar es Salaam jana kuhusu taarifa yake ya kwanza baada ya kuteuliwa tena na Rais Samia Suluhu Hassan kushika wadhifa huo.

Alisema kuwa kuanzia Mei hadi Novemba mwaka huu, kulikuwa na kiwango cha shehena cha tani milioni 14.4 zilizohudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam sawa na ongezeko la asilimia 5.6 kulinganishwa na shehena ya tani milioni 13.7 iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Tangu DP World ianze kufanya kazi Aprili 2024, katika kipindi cha miezi mitano tu tayari imeshawekeza Sh. bilioni 214.425 katika ya Sh. bilioni 665 inazopaswa kuwekeza katika kipindi cha miaka mitano ya mwanzo ya mkataba walioingia nao.

Msigwa ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, alisema kupitia mkataba wa TPA na kampuni ya DP World Dar es Salaam, ukarabati wa mitambo iliyokuwa ya TPA umeshafanyika sambamba na usimikaji wa mifumo mipya ya Tehama.

Alisema uwekezaji huo pia umepunguza muda wa meli kusubiri kutoka siku 46 hadi 70 ilivyokuwa awali hadi wastani wa siku saba, hivyo kuokoa mabilioni ya shilingi ambayo TPA ilikuwa inalipa kwa wenye meli kutokana na meli zao kukaa muda mrefu kusubiri kushusha mzigo.

"Kuna meli sasa hazisubiri kabisa, meli za makasha hakuna kusubiri kabisa, ni kufika na kushusha na kuondoka," alisema Msigwa na kubainisha kuwa hata muda wa kuhudumia meli za makasha gatini kutokana na vitendea kazi vya kisasa ambavyo kampuni hiyo ya Falme za Kiarabu imewekeza nchini umepungua.

Msigwa alisema kuwa hata gharama za uendeshaji zimepungua kwa asilimia 2.5 ya makusanyo, wakati awali bandari hiyo ilijiendesha kwa hasara huku serikali ikipata mapato ya Sh. bilioni 325.3.

Alisema mapato ya TPA nayo yameongezeka, yakifikia Sh. trilioni moja kutoka Sh. bilioni 850 walizokuwa wanakusanya awali.

Msemaji Mkuu huyo alisema wafanyabiashara waliokuwa wameihama bandari hiyo wamerejea kwa kasi huku uwekezaji ukiongezeka nchini.

"Katika kuvutia wawekezaji wengi zaidi, mtaona hivi karibuni tutaongeza gati, kuboresha reli ya TAZARA, bandari kavu. Sekta binafsi haiepukiki katika kuendesha bandari," alisema.

**SGR**

Kuhusu mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), Msigwa alisema wanaendelea na utekelezaji mradi huo kwa vipande vyote vinane na kuwaomba wananchi wapuuze madai kwamba makandarasi wameondoka eneo la mradi kutokana na serikali kukosa fedha.

Alisema tayari mradi huo unafanya vizuri katika ruti walizozindua za Dar es Salaam - Dodoma na Morogoro - Dar es Salaam, abiria 1,174,404 wakihudumiwa hadi kufikia Desemba 11 mwaka huu.

Alisema idadi hiyo ya abiria ni zaidi ya mara mbili ya wanaosafiri kwa treni za kawaida kwa mwaka, akibainisha kuwa treni hizo hubeba wastani wa abiria 400,000 tu kwa mwaka mzima.

Hata hivyo, Msigwa alisema mapato makubwa ya mradi huo wanatarajia kuyapata watakapoanza kusafirisha mizigo kwa treni za mizigo.

Msigwa alitumia nafasi hiyo kutoa onyo kwa wanaohujumu miundombinu ya SGR, akisisitiza hakuna atayekwepa kukamatwa baada ya kufanya hujuma yoyote kwa kuwa eneo lote la miundombinu hiyo linalindwa kwa kutumia kamera na mifumo mingine ya kiintelijensia.

Alidokeza kuwa mpango uliopo ni kuhakikisha wanatumia pia kamera za satelaiti ili kuwa na ufanisi zaidi katika kunasa wahujumu.

> **"Katika kuvutia wawekezaji wengi zaidi, mtaona hivi karibuni tutaongeza gati, kuboresha reli ya TAZARA, bandari kavu. Sekta binafsi haiepukiki katika kuendesha bandari,"**

**MWENDOKASI**

Akizungumzia Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, Msigwa alisema kuwa hivi sasa kunashuhudiwa foleni mkoani Dar es Salaam kutokana na barabara nyingi kuwa katika ujenzi wa miundombinu ya mradi huo.


Alisema kuwa muda si mrefu mabasi ya mwendokasi yataanza kutoa huduma katika barabara iliyokamilika kutoka Gerezani hadi Mbagala.

Alisema mradi huo una manufaa makubwa kwa serikali na wananchi, akifafanua kuwa awali mtu alitumia hadi Sh. 20,000 kwa nauli kutoka Kimara hadi Posta, lakini hivi sasa anatumia Sh. 1,500, Sh. 750 kwenda kazini na Sh. 750 nyingine kurejea nyumbani kwake.

Alisema kuwa kwa takwimu za mwaka 2015, foleni Dar es Salaam zilikuwa zinasababisha hasara ya Sh. bilioni nne kwa siku, hivyo mradi huo ni muhimu kuepuka hasara hiyo.

Msigwa alitaja faida nyingine ya mradi huo ni kupunguza magari mengi kuwa barabarani. Hivyo kuepusha uchafuzi wa mazingira.

Katika mkutano huo, Msigwa pia alizungumzia maendeleo ya Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), upatikanaji wa mbolea nchini na ruzuku inayotolewa na serikali, pia masuala ya utamaduni, sanaa, michezo na Sekta ya Habari anakotoka.




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA IRINGA, MBEYA NA DODOMA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Dodoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa tarehe 27 Desemba, 2024 hadi 02 Januari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Ijumaa tarehe 27 Desemba, 2024 hadi Alhamisi tarehe 02 Januari, 2025.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 8 na kubonyeza, baada ya hapo atachagua namba 2 na kubonyeza, Kisha atachagua Namba 3 (Tume Huru ya Uchaguzi) na hapo, atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

**Limetolewa tarehe 19 Desemba, 2024 na:**

**Saida Hilal Mohammed**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

2183O2902

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wafanyabiashara lindeni afya za wateja wenu

**WAFANYABIASHARA** wa vipodozi wanajukumu kubwa kuhakikisha wateja wao wanakuwa salama kwa kutumia bidhaa wanazouza bila kupata madhara.

Lakini baadhi yao wamekuwa wakiingiza vipodozi vyenye viambata vya sumu na kusababisha watu kuharibika ngozi na hatimaye kupata magonjwa ya saratani.

Pamoja na serikali kupiga marufuku uingizaji wa bidhaa za vipodozi vyenye viambata vya sumu, lakini baadhi ya wafanyabiashara hao hutumia njia za panya kuziingiza nchini.

Hata uuzaji wake huwa ni wa siri na wanaowauzia ni wateja wao waliowazoea.

Kuna maduka katika baadhi ya sehemu hufunguliwa nyakati za usiku pekee ili kuuza vipodozi hivyo na wateja wao wanayajua yalipo.

Hii ni hatari kwa sababu wananchi wanaendelea kuathirika kwa kukosa uelewa wa kutumia bidhaa hizo zilizopigwa marufuku.

Katika kukabiliana na suala hilo, Shirika la Viwango Nchini (TBS), limewataka watu wote wanaofanyabiashara ya chakula na vipodozi kusajili maeneo yao ili iwe rahisi kukaguliwa kwa ajili ya usalama wa afya za wananchi.

Vile vile, shirika limewataka wafanyabiashara na watumiaji wa bidhaa kuhakikisha bidhaa wanazonunua zina nembo ya alama ya ubora.

TBS imesisitiza kuwa wanaofanyabiashara ya vipodozi wanapaswa kuhakikisha vipodozi hivyo havina viambata sumu vyenye madhara kwa afya za watumiaji.

Watumiaji wa vipodozi hivyo mara nyingi hupenda kubadili ngozi zao na kutaka kufanana na watu weupe bila kujua athari zake.

Wengi wanaotumia baadaye ngozi zao hupata madhara kiasi cha kushindwa kutembea kwenye jua kwa sababu ngozi zao zinakuwa zimeshaathirika.

Wengine hulazimika kutembea na miamvuli kujikinga na jua lisipenye moja kwa moja kwenye ngozi zao.

Madhara ya vipodozi hivyo pia ni ngozi kuungua na badala ya kupata rangi wanayoitaka huwa wekundu na hatimaye weusi kama rangi ya mkaa.

Pamoja na elimu ya kuwataka wananchi kuacha kutumia vipodozi vyenye viambata vya sumu, lakini ni kama inawashawishi kuendelea kutumia kwa kutaka kubadili ngozi waliyozaliwa nayo na kuiga rangi za watu weupe.

Mara kwa mara tumeshuhudia TBS ikiteketeza tani kwa tani za vipodozi vyenye viambata vya sumu, lakini wafanyabishara wanaendelea kuviingiza na kuangamiza maisha ya wananchi wenzao.

Na kwa wanaotumia bidhaa hizo wakumbuke kuwa urembo sio mtu kuwa mweupe, hata hao wenye rangi nyeupe wanatamani wawe weusi, lakini wanashindwa wataipataje.

Ndio maana hao wanaoonekana kuwa warembo kwa sababu ya rangi zao nyeupe, wanajianika kwenye jua ili wapate rangi nyeusi.

Ni lazima kabla ya kuiga kitu mtu afahamu faida na hasara zake kabla ya kuamua kukifanya.

TBS ina kazi kubwa ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduka yanayouza vipodozi ili kuwabaini wanaoendelea kuviingiza.


Na wenye viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo pia wanapaswa kukaguliwa ili kujiridhisha wanazalisha kwa ubora unaotakiwa.

Kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha na mifumo ya kimenejimenti na kusajili bidhaa za chakula na vipodozi.

Wanunuzi wa bidhaa hizo pia wanatakiwa kuthibitisha kuwa zina nembo ya uhakiki wa TBS ili kuwa na uhakika kwamba ni yenye ubora na ikitumiwa haileti madhara kwa mtumiaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Bodaboda na mbwembwe hizi mpya barabarani, vifo vyaja

**KAZI** ya kuendesha pikipiki ambazo ni maarufu kama 'bodaboda', ni biashara pia ni ajira kama zilivyo ajira nyingine halali zinazowaingizia watu vipato vya kuendeshea maisha yao ya kila siku.

Hata hivyo, baadhi ya vijana ambao wameingia katika ajira hiyo ni kama wamekuwa wazito kuelewa umuhimu wa ajira hiyo na kuiheshimu ili iweze kuwanufaisha wao na familia zao.

Kwanini? Kwa sababu kila uchao wamekuwa wakiibuka na mitindo ambayo ni hatari kwa maisha yao, aidha kwa kuelewa au kutoelewa madhara ya kile wanachokifanya wawapo barabarani.

Wamekuja na mtindo ambao inawezekana wanauona ni wa kawaida, lakini ukweli ni kwamba unaweza kuwasababishia madhara makubwa iwapo wataendelea nao au wasipodhibitiwa.

Mtindo wenyewe ni wa kutawala barabara na kuendesha bodaboda kwa fujo bila tahadhari huku wakifanya vituko vya kuachia usukani, wanapokuwa katika msafara wa kusindikiza mwenzao aliyefariki dunia au mambo yanayofanana na hayo.

Wakati mwingine, baadhi yao hubebana hata wanne kwenye bodaboda moja, wengine wakiendesha huku wamesimama. Yaani hufanya kila aina ya vituko barabarani, ambavyo ni hatari kwa usalama wao.

Vilevile, kuna kero ambayo madereva hao wanachangia ya kutawala pande zote za barabara kwa muda na kusababisha watu wengine washindwe kuitumia kana kwamba ni mali yao.

Sijui mikoa mingine, lakini kwa Dar es Salaam imekuwa kama jambo la kawaida kusikia honi nyingi zikipigwa pale wanapokuwa wakisindikiza msafara wa msiba wa mwenzao huku wametanda barabara yote.

Kwa ujumla ni kwamba wanajiweka katika mazingira ya kuhatarisha maisha yao na pia wanasababisha kero kwa watumiaji wengine wa barabara. Hivyo, ingependeza kama watadhibitiwa.

Nilidhani kwamba mwenzao anapopoteza maisha, ni wakati mwafaka kwao kutafakari na kuchukua tahadhari zaidi wawapo barabarani, lakini ajabu wanaendelea kujiweka katika mazingira hatarishi.

Yawezekana aliyefariki atakuwa amesababishiwa ajali au amesababisha mwenyewe, lakini bado wanapaswa kutambua kuwa umakini unahitajika wawapo barabarani, sio kujiendea wanavyotaka.

Udereva wa bodaboda ni ajira ambayo imesaidia vijana kuacha kushinda vijiweni, lakini bahati mbaya baadhi yao wanashindwa kuheshimu ajira hiyo na kusababisha ionekane kama kazi ya kihuni.

Kutoheshimu ajira hiyo kunachangia kuwapo kwa ajali nyingi zinazogharimu maisha yao na ya abiria, kwani baadhi yao huwa wanatuhumiwa kujihusisha na ulevi wa pombe wawapo kazini.

Inaelezwa kuwa ajali za bodanoda bado ni tishio, kwani Taasisi ya Tiba na Mifupa (MOI), inasema inapokea wagonjwa takriban 700 kwa mwezi huku asilimia 60 ya wagonjwa hao wakitokana na ajali za bodaboda.

Hayo ni kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi wa MOI), Dk.Lemeri Mchome, alipoitoa wakati fulani akipokea msaada wa vifaa mbalimbali vya tiba, kutoka kwa wadau wa afya.

Kwa taarifa hiyo, ni wazi kwamba kuna ombwe kwa madereva wa bodaboda la kutokuwa makini wawapo katika ajira hiyo na kujisababishia madhara au kuwasababishia abiria wao.

Jambo ambalo angalau sasa wanaliheshimu, ni kutojichukulia sheria mkononi kama zamani walipokuwa wakiona mwenzao amegongwa na gari wanavamia na kutembeza kipigo bila kujua chanzo cha ajali.

Lakini wizi, kutotii sheria za usalama barabarani kama kutovaa kofia ngumu, kulewa, kubeba abiria zaidi ya mmoja, kuvuka katika makutano ya barabara bila kuruhusiwa na taa, hayo yanaendelea kama kawaida.

Ukweli ni kwamba bodaboda zimeongeza ajira, kurahisisha usafiri maeneo ya mijini na vijijini, lakini tatizo ni wahusika kushindwa kuheshimu kazi hiyo na kusababisha wao kama nguvukazi ya taifa kupotea bure.

# Bashungwa akunwa utendaji kazi NIDA

**Na Kulwa Mzee**

> **"Natoa rai kwa NIDA kuhakikisha ndani ya miezi miwili mnasambaza vitambulisho vyote vilivyotengenezwa kwa wahusika ili wavitumie kwa matumizi yao ... mbalimbali,"**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Innocent Bashungwa, amesema kwa sasa anafurahishwa na utendaji kazi wa kituo cha uchakataji taarifa za utambulisho wa taifa cha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kilichoko Kibaha mkoani Pwani.

Alisema hayo jana wakati akizindua magari mapya manane aina ya Toyota Landcruisser Hardtop kati ya 20 yaliyoagizwa yakiwa na thamani ya Sh. bilioni 2.2 na mengine 12 yaliyosalia yatawasili hivi karibuni.

"Licha ya magari hayo 20, nimeambiwa mmetenga Sh. bilioni 2.1 kwa ajili ya ununuzi wa magari mengine 10 katika bajeti ya mwaka huu wa fedha wa 2024/2025," alisema Bashungwa.

Waziri Bashungwa kabla ya kuzindua magari hayo katika ofisi za makao makuu ya NIDA, Dar es Salaam, alitembelea ofisi mbalimbali za mamlaka hiyo ikiwamo ya Kibaha.

"Nimefurahishwa na utendaji kazi wa kituo kwa sasa na pia kama serikali tutahakikisha changamoto mbalimbali za usafiri zitatatuliwa haraka iwezekanavyo," alisema.

Waziri Bashungwa pia aliwataka vijana kuchangamkia fursa ya kujiandikisha kwa hiari katika mamlaka hiyo ili kuwa na vigezo vitakavyowawezesha kujiunga na vyuo vikuu, kupata mikopo na fursa mbalimbali za kazi za ndani na nje ya nchi.

"Natoa rai kwa NIDA kuhakikisha ndani ya miezi miwili mnasambaza vitambulisho vyote vilivyotengenezwa kwa wahusika ili wavitumie kwa matumizi yao mbalimbali," alisisitiza Bashungwa.

"Namshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga Sh bilioni 42.5 kwa ajili ya utendaji kazi wa mamlaka katika mwaka huu wa fedha wa 2024/25.

"Kuhusu changamoto za kifedha zinazoikabili NIDA, nitazungumza na Hazina ili kuona namna bora ya kuzitatua na kufanikisha mchakato wa utoaji wa vitambulisho kwa wananchi," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, Deusdedit Buberwa, aliishukuru serikali kwa kukabidhi magari hayo na kuahidi kuwa yatatunzwa na yatatumika kwa kazi iliyokusudiwa.

"Magari haya yatatusaidia kwa ajili ya kazi kubwa mbili kama vile kusajili wananchi pamoja na kusambaza vitambulisho kama alivyosema Mheshimiwa Waziri hivi punde," alisema Buberwa.

Alisema jiografia ya Tanzania inatofautiana kutoka sehemu moja mpaka nyingine hivyo magari hayo yatarahisisha kazi yao kwa kiasi kikubwa na kuweza kutimiza malengo ya kuhakikisha kila Mtanzania anapata kitambulisho cha taifa.

"Kwa upande wa vitambulisho mpaka Novemba 2024, tulikuwa tumekwisha sajili jumla ya watu zaidi ya milioni 25, kati ya hao tayari wananchi milioni 21 wamekwishapatiwa namba za utambulisho,"

# Bodi ya NBAA yatakiwa kupitia upya mitaala

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, ameiagiza Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) kupitia upya mitaala iliyopo kwa ajili ya uboreshaji wa taaluma inayotolewa na taasisi hiyo kwa manufaa ya taifa na wananchi wake.

Rai hiyo ilitolewa juzi katika ukumbi wa Mikutano wa APC Bunju, Dar es Salaam, wakati akizindua bodi mpya ya NBAA itakayofanya kazi kwa kipindi cha miaka mitatu hadi 2027.

Chande alisema kazi kubwa ya bodi hiyo ni kusimamia na kukuza tasinia ya uhasibu nchini ili kuhakikisha inatoa mchango stahili katika kukuza uchumi kupitia huduma za kihasibu na ukaguzi wa hesabu za ndani katika taasisi na mashirika mbalimbali.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameidhinisha Sh. bilioni 29.8 kati ya Sh. bilioni 30 zilizoombwa na bodi hiyo kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho Dodoma na anaamini watajenga ofisi nzuri na ya kisasa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa NBAA, CPA Prof. Sylivia Temu, alisema Mwenyekiti aliyeteuliwa na Rais na wajumbe walioteuliwa na Waziri wa Fedha, wana kazi ya kuhakikisha wanachama wanazingatia vigezo vya kimataifa katika kuandaa hesabu ambazo zinatumiwa na wadau mbalimbali.

Pia alisema bodi ina kazi ya kuhakikisha wakaguzi wa hesabu wanazingatia vigezo vya kimataifa ili kutoa taarifa zinazoaminika kwa wawekezaji ili kuendeleza jitihada chanya za maendeleo ya nchi katika nyanja mbalimbali ikiwamo ya uchumi.

"Nchi yetu inakuwa na sasa iko katika uchumi wa kati wa ngazi ya chini. Sisi kama wahasibu tunaungana na juhudi za serikali katika kutoa taarifa za kihesabu zinazoaminika zitakazowavutia wawekezaji ili kuondoa shaka katika suala la uwekezaji.

Prof. Temu alisema kuwa bodi ya NBAA itatekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Naibu Waziri kwa kuwa yanachochea utendaji kazi na kuleta ufanisi wenye tija kwa taifa.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA FEDHA**

**MWALIKO KWA WADAU WA KUSHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA KIKOSI KAZI CHA MABORESHO YA SERA ZA KODI (TASK FORCE ON TAX REFORMS) KWA AJILI YA MATAYARISHO YA BAJETI YA 2025/26**

Kamati ya Maboresho ya Sera za Kodi (Task Force on Tax Reforms) inayohusika na matayarisho ya Bajeti ya Serikali 2025/26 itaanza kazi yake mwezi Februari 2025. Vikao kazi vya Kamati vitazinduliwa na Kongamano la Kodi na Uwekezaji Kitaifa ambalo litafanyika mwezi Januari 2025.

Kila mwaka, Kamati hii, imekuwa ikipokea maoni ya wadau, kufanya uchambuzi, na kufanikisha majadiliano ya masuala mbalimbali yanayohusiana na sera za kodi na usimamizi wake. Maoni hayo yamekuwa na mchango mkubwa katika uandaaji wa sera na yamesaidia katika kuunda mfumo wa kodi ambao umewezesha utatuzi wa masuala mbalimbali ya kodi kwa ufasaha na uwazi.

Malengo ya sera za kodi kwa mwaka 2025/26 ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuvutia uwekezaji; kuwezesha ukuaji wa biashara ndogondogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi; kuimarisha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari; upanuzi wa wigo wa kodi; kuongeza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika usimamizi wa kodi; kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi; na kuweka utaratibu mzuri wa ulipaji wa ada na tozo mbalimbali.

Ili kufanikisha kazi hiyo, Kamati inakaribisha ushiriki wa taasisi za Serikali, sekta binafsi, asasi zisizo za Serikali, taasisi za dini, jamii ya wasomi, taasisi za utafiti na wataalamu wengine katika sekta ya uchumi kwa kutoa maoni ya kuboresha sera za kodi kwa maandishi. Maoni hayo yanapaswa kuonesha yafuatayo:

i. Biashara, kampuni, taasisi, chama/vyama au makundi ambayo yanawakilisha;
ii. Mapendekezo ya mabadiliko ya kisera na mapato ya Serikali yanayotokana na kodi na yasiyo ya kodi, ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa sekta, maeneo au aina ya walipakodi ambao wataathirika, na kwa namna watakavyoathirika;
iii. Makisio ya athari kwenye uchumi na mapato ya Serikali katika mwaka huu wa utekelezaji na katika miaka ijayo;
iv. Sababu za mapendekezo ya mabadiliko kwenye sera za mapato, hususan uchambuzi wa namna ambavyo mapendekezo hayo yataisaidia Serikali kufanikisha malengo yake makuu; na
v. Pale ambapo mapendekezo yanapunguza mapato ya Serikali (hata katika kipindi cha muda mfupi), mapendekezo hayo yaoneshe bayana hatua za kufidia upungufu wa mapato ambao utajitokeza.

Kamati inatarajia kupata mapendekezo yatakayowezesha majadiliano yenye tija kati ya Serikali na Wadau.

Mapendekezo yawasilishwe kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi tarehe **31 Machi 2025** kupitia lango (portal) lifuatalo: **https://maoni.mof.go.tz/. Maoni yatakayowasilishwa baada ya tarehe ya mwisho hayatapokelewa.**

Mapendekezo yanaweza pia kuwasilishwa kwa anuani ifuatayo:
**Sekretariati ya Kamati ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi,**

**Wizara ya Fedha,**
**Idara ya Uchambuzi wa Sera,**
**Jengo la Hazina (Ghorofa ya Pili),**
**18 Barabara ya Jakaya Kikwete,**
**S.L.P 2802,**
**DODOMA.**
**AU**
Barua Pepe: **mathias.kadebe@hazina.go.tz au salha.mzee@hazina.go.tz**

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na Mathias Kadebe 0713 694 895; au Salha Mzee 0652 442 944.
Pia tembelea tovuti yetu: www.mof.go.tz.

**Tangazo hili limetolewa na:**

**KATIBU MKUU - HAZINA**
**Desemba, 2024**

218298402

# Wazalishaji bidhaa watakiwa kuthibitisha mifumo ya ubora

**Na Joseph Mwendapole**

WAZALISHAJI wenye viwanda vikubwa na vidogo nchini wameshauriwa kuthibitisha mifumo ya usimamizi wa ubora kwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili kufikia kwa urahisi masoko ya kitaifa na kimataifa.

Meneja wa Kuthibitisha Mifumo ya Usimamizi wa Ubora wa (TBS), Nasra Yusuf, alisema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye ofisi za shirika hilo.

Alisema iwapo wazalishaji wakubwa na wadogo watathibitisha mifumo yao itakuwa rahisi kwao kuaminika kwenye masoko mbalimbali duniani kuhusu usalama na ubora wa bidhaa zao.

"Na wanapaswa kujua kwamba wajibu wa kuthibitisha mifumo ya ubora ni kwa wote yaani wazalishaji wakubwa na wadogo na hii itawasaidia kuepuka hasara kwenye shughuli zao za uzalishaji kwasababu watakuwa wanafuata mifumo ya ubora iliyothibitishwa," alisema.

Alisema kitengo hicho kinatoa huduma za kuthibitisha ubora kwa kufuata viwango vya kimataifa yaani ISO 9001 kwa sekta binafsi viwanda na wazalishaji wengine.

Yusuf alisema mfumo mwingine unaopaswa kuthibitishwa na TBS ni wa usalama wa chakula kwa wazalishaji na wasambazaji wa chakula na kuongeza kuwa mfumo mwingine wanaopaswa kuuthibitisha ni mfumo wa usimamizi wa mazingira.

"Mfumo huu wa usimamizi wa mazingira ni muhimu sana kwa sababu wazalishaji wengi wakati wa shughuli zao wanaacha athari kwa mazingira. Mfumo mwingine unaopaswa kuthibitishwa ni ule wa usalama sehemu ya kazi unaohusisha taasisi na kampuni zote kwani tunafahamu umuhimu wa usalama kazini," alisema.

Alitaja faida zinazopatikana kwa wazalishaji kuthibitisha mifumo kuwa ni kuwa na uthabiti wa kutoa huduma zao ukiwa umethibitishwa mfumo utakuwa na huduma zenye ubora wakati wote na kuwapa uhakika wa kuaminiwa na wateja wao wakati wote.

"Faida nyingine ni uhakika wa masoko ya ndani na nje ya nchi kwasababu huduma wanazotoa zitakuwa zimethibitishwa ubora kwa hiyo tunaomba kutumia nafasi hii kuwaomba wazalishaji wathibitishe mifumo yao kwenye shirika kama sheria inavyotaka," alisema.

Naye Meneja Usajili wa Biashara na Majengo wa TBS, Habakuki Kalebo, alisema TBS imeingia makubaliano na halmashauri 184 nchini kufanya kazi ya kusajili maeneo yanayotoa huduma ya chakula.

"Tumefanikiwa kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi kwa kutumia halimashauri zote nchini tunazofanya nazo kazi ambapo wamefanikiwa kusajili maeneo yao ya biashara na wanapata huduma zingine kwa karibu," alisema Kalebo.

Alisema TBS huwa inafanya ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha bidhaa zote zinazoingia nchini zimepewa alama ya ubora na zile zinazoingia kinyume na utaratibu na zikaonekana kuwa na viambata vya sumu kama vipodozi shirika hutoa taarifa kwa umma ili kujiepusha na kuzitumia.

"Kila mwezi huwa tunahuisha taarifa zetu kwenye wavuti yetu ambapo wananchi wanaweza kuingia na kuangalia bidhaa ambazo zimepigwa marufuku kuuzwa kwasababu zina viambata vya sumu kwa hiyo tunaomba wananchi kabla ya kununua bidhaa waangalie kama bidhaa hizo zimeruhusiwa kuuzwa nchini kwasabau huwa tunaweka kwenye wavuti yetu," alisema.



Mwenyekiti wa serikali ya kitongoji cha Majengo kata ya Majengo wilayani Muheza Tanga, Seif Twenye (kulia) akimwonesha mwananchi karavati linalojengwa katika barabara ya mtaa wa Kitiku jana, ambapo ujenzi huo unaendeshwa na TARURA wilaya. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Siri ufaulu wanafunzi darasani yabainishwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

NAIBU Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu ya Msingi katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dk. Wilson Mahera, amesema bila kuwa na walimu bora, mejengo mazuri, vitabu na vifaa ni ndoto kufikia malengo ya elimu.

Dk. Mahera aliyasema hayo juzi alipokuwa akifungua mafunzo ya matumizi bora ya vifaa vya teknolojia ya Habari na mawasilino (TEHAMA) kwa waratibu wa elimu na walimu wakuu wa shule za msingi kutoka mikoa ya Njombe, Mbeya, Songwe, Iringa na Ruvuma.

Alisema walimu wakuu wanatakiwa kuvijua vikwazo vya walimu wengine na kuvishughulikia kwa kuwa kwa kufanya hivyo, watasaidia kuwa na walimu bora watakaoongeza ufaulu kwenye shule zao.

"Tusipokuwa na uongozi mzuri walimu wengine hawawezi kufundisha vizuri na tunaweza tusipate mafanikio tunayoyataka kama tunavyotarajia," alisema.

Kuhusu mafunzo hayo, Dk. Mahera alisema tehama kwasasa ni muhimu kulingana na mabadiliko ya maendeleo ya sasa. Hivyo walimu wanatakiwa kuzingatia mafunzo hayo na kufanyia kazi.

Dk. Mahera alisema wanafunzi wa shule za msingi wanatakiwa kufundishwa TEHAMA ili wanapofika sekondari waendelee kuimarika na kuwa na uwezo wa kujiajiri baadaye. "Vijana wengi wamejiajiri kupitia TEHAMA ndiyo maana elimu hiyo inapewa kipaumbele ili wakifika sekondari wanaendelea na somo hilo litakalowasaidia kujiajiri wakiwa uraiani. Pia nchi zingine kwa sasa zimeendelea katika TEHAMA, hivyo inabidi twende sambamba nao," alisema.

Aliwataka walimu kuhakikisha vifaa vya Tehama vinavyonunuliwa vinatumika na wanafunzi wanufaike na elimu hiyo isiwe kama nyakati zilizopita ambapo baadhi ya vifaa hivyo vilikuwa havitumiki.

Mratibu wa mradi wa BOOST kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Lawrence Raphael, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuboresha umahiri wa elimu katika ufundishaji na ujifunzaji somo la TEHEMA.

Naye Mkurugenzi wa Kudhibiti Ubora wa Shule kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ephraim Simbeye, alisema baada ya mafunzo hayo watawafuatilia walimu walionufaika na kuona maendeleo yao.

# Vijana wafundwa kufanya kazi kwa bidii

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MJUMBE wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Iringa, Dickson Mwipopo, ametaka Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Wilaya ya Iringa Mjini kufanya kazi kwa bidii, ikiwamo kujikita kwenye kilimo, ili kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Akizungumza juzi katika kongamano la kuwashukuru vijana wa CCM wa wilaya hiyo kwa kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Mwipopo aliwataka vijana kuacha kutegemea misaada, badala yake wajitegemee kwa kufanya kazi kwa juhudi.

Mwipopo alisema Rais Samia Suluhu Hassan amewekeza zaidi ya Sh. bilioni 56 katika ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ili kuboresha sekta ya kilimo na kuwawezesha vijana kujikita katika kilimo biashara.

Alisema mradi huo unapaswa kutumiwa na wakazi wa Iringa badala ya kusubiri watu kutoka mikoa mingine kama Mbeya au Morogoro kutumia fursa hizo.

"Vijana tuache kusubiri kupewa. Rais Samia ametuletea skimu ya kilimo. Twendeni tukafanye kazi kwa bidii. Iringa tuna sifa ya kufanya kazi, tusikubali kurudi nyuma," alisema.

Aidha, aliwataka vijana kuchangamkia mafunzo ya ujuzi mbalimbali ili waweze kujiajiri na kuwa na maisha endelevu badala ya kulalamikia ukosefu wa ajira.

Mwenyekiti wa CCM (UVCCM) Wilaya ya Iringa Mjini, Isack Kikoti, alisema vijana walijitokeza kwa wingi na kushiriki kikamilifu katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Alisema CCM ilishinda mitaa yote 192 ya Iringa Mjini na kuonyesha nguvu ya ushirikiano wa vijana.

"Tumemaliza salama uchaguzi wa serikali za mitaa lakini hii ni ishara ya maandalizi yetu kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Tutahakikisha tunazalisha ushindi mkubwa kwa Rais, wabunge na madiwani," alisema.

Kikoti pia alitoa wito kwa vijana kuanza maandalizi ya uchaguzi kwa kuwahamasisha wananchi kujitokeza kuhakiki na kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura.

Kikoti alikiri kuwa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) bado haujawa na miradi ya kiuchumi inayomilikiwa na vijana. Alisema kuwa hali hiyo imewafanya vijana kuwa ombaomba, jambo ambalo alisema linahitaji kutatuliwa.

Hata hivyo aliomba msaada wa kukamilishwa kwa ujenzi wa nyumba ya katibu wa UVCCM ambayo ilisimama kutokana na changamoto za kiuchumi.

Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Iringa, Tumaini Msowoya, aliwahimiza vijana waliomaliza vyuo vikuu kujiajiri badala ya kutegemea ajira. Alisisitiza kuwa nidhamu ni msingi wa mafanikio katika maisha, kazi na biashara.

"Vijana wenzangu, nidhamu ndio msingi wa mafanikio. Bila nidhamu, huwezi kufanya kazi au biashara kwa ufanisi. Hakikisha unajenga tabia ya nidhamu katika kila hatua ya maisha yako," alisema.

Alitaka vijana kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya taifa kwa kufanya kazi kwa bidii, kujiajiri na kudumisha nidhamu na mshikamano kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.



# TAKUKURU yawapa msaada njiti

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), imeikabidhi Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru mashine ya kukuzia watoto wanaozaliwa kabla ya muda (njiti) yenye thamani ya Sh. milioni tisa.

Vilevile, imekabidhi stakabadhi ya Sh. milioni 2.755 iliyolipwa katika Bohari Kuu ya Dawa nchini (MSD) kwa ajili ya ununuzi wa dawa na pampasi kuwasaidia wahitaji hao.

Akikabidhi misaada hiyo jana, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Crispin Chalamila alisema wamekabidhi mashine hiyo mahusus i kwa ajili ya kuwatia joto watoto ili waendelee kupata makuzi bora.

"Tuko hapa Arusha kwa siku tatu nne kwa mkutano, kwa namna yeyote na sisi tushiriki kutatua au kupunguza baadhi ya changamoto katika hospitali hii," alisema.

> **"Tuko hapa Arusha kwa siku tatu nne kwa mkutano, kwa namna yeyote na sisi tushiriki kutatua au kupunguza baadhi ya changamoto...**

Tumechangishana, tukanunua hii mashine, ambayo nina furaha kukabidhi kwa niaba ya watumishi wa TAKUKURU," aliendelea kusema.

Akipokeza misaada hiyo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Alex Ernest, alishukuru TAKUKURU kwa moyo wao wa upendo kwa kuwafikiria wahitaji.

"Napenda niwashukuru kwa dhati kwa msaada huu, kwetu ni mkubwa sana. Hospitali yetu ya Rufani ya Mkoa wa Arusha, inapokea wagonjwa wengi, tuna takribani watoto 100 tunawalaza kwenye wodi ya njiti, ambao wamezaliwa kabla ya kutumiza umri," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Alex, watoto hao wana mahitaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na baadhi ya vifaa ambavyo TAKUKURU imekabidhi kusaidia kutengeneza joto la mwili.

"Kifaa hiki ambacho mmekitoa ni muhimu sana na ni msaada mkubwa sana na ni moja kati ya vifaa ambayo tutavitumia kuokoa maisha ya watoto hawa njiti,"alisisitiza.



Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania wa Chama Cha Mapinduzi likiongozwa na Mwenyekiti wake, Mary Chatanda, Katibu Mkuu, Susan Kunambi na Kamati ya utekelezaji taifa wakiwa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga Balozi Batilda Burian, wakitembelea Mapango ya Amboni mkoani Tanga hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara yavalia njuga kesi sugu wasakwa

**Na Allan Isack**, ARUSHA

WIZARA ya Sheria na Katiba imesema itahakikisha kesi za ukatili wa kijinsia, migogoro ya wakulima na wafugaji na uhifadhi wa dunia zinamalizika kwa wakati na kutoa haki kwa wakati.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Damas Ndumbaro wakati wa ziara yake katika taasisi zilizopo chini ya wizara yake mkoani hapa.

Taasisi hizo ni Ofisi ya Mashtaka ya Taifa (NPS) , Makao Makuu ya Polisi, Kituo Kikuu cha Polisi, Kituo cha Polisi Muriet na Mahabusu ya Watoto.

Alisema kesi hizo tatu ikiwemo uhifadhi dunia kula malalamiko lukuki ya uharibifu wa mazingira na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

"Tusipos imamia uhifadhi na tukiruhusu wanyamapori wauawe tunakwenda kubaya, hicho ni kipaumbele kwa sisi tunaohudumu kwenye sekta ya sheria na haki," alisema na kuongeza kuwa:.

"Malalamiko ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto yamekuwa makubwa kwa kuwa kesi zimeongezeka na kazi ya sheria ni kutatua matatizo na tumejipanga kutumia nguvu za kisheria kupambana na hilo."

Akizungumzia kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji, alisema imekuwa donda ndugu na kuhatarisha amani ya nchi na wananchi wanaishi katika maeneo inakotokea.

Ndumbaro, alisema tatizo hilo nalo wameamua kulipa kipaumbele ili kuhakikisha migogoro hiyo inakwisha nchini.

Hata hivyo, alisema NPS, wameboresha utoaji huduma kwa kuweka ukomo wa kusikiliza kesi kati ya miezi sita na mwaka mmoja badala ya kuvuka miaka miwili kama ambavyo imekuwa ikitokea.

"Huo ni utendaji ulioboreshwa sana pamoja na kiwango cha kushinda kesi hizo kimeongezeka," alisema.

Aliwataka waendesha mashtaka na mawakili wa serikali kumaliza kesi kwa wakati ili haki itendeke na kuondoa manung'uniko kwa jamii.

Renatus Mkude, Mkurugenzi Msaidizi Makosa dhidi ya Binadamu na Utenga NPS, alisema Ndumbaro amefanya ziara mkoani hapa kutembelea taasisi zilizopo chini ya wizara hiyo na ambazo wanashirikiana nazo kwa ngazi ya mkoa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 24 cha sheria ya mashtaka nchini, Mkurugenzi wa Mashtaka, taasisi hizo na NPS wana jukumu la kuratibu upelelezi katika vyombo chunguzi.

# Serikali yapongezwa kuboresha Bandari ya Tanga

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

UMOJA wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) nchini, umeipongeza serikali kwa kutekekeza mradi wa kimkakati wa kuboresha miundombinu katika Bandari ya Tanga.

Pongezi hizo zilitolewa mwanzoni mwa wiki hii wakati wa ziara ya Wajumbe wa Baraza Kuu la UWT katika Bandari ya Tanga.

Akizungumza baada ya kupata maelekezo kutoka kwa viongozi waandamizi wa bandari hiyo, Mwenyekiti wa UWT Taifa Mary Pius Chatanda, alisema umoja huo kupitia wajumbe wa baraza kuu mikoa yote nchini, itaendelea kutangaza kazi kubwa na nzuri zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kuimarisha uchumi nchini na mwananchi mmoja mmoja.

"Ni wazi kuwa Mkoa wa Tanga unaimarika kiuchumi, mradi huu wa uboreshaji wa Bandari ya Tanga utainua uchumi wa mikoa ya Kaskazini na nchi kwa ujumla," alisema.

Alisema maboresho hayo yenye thamani ya shilingi Bilioni 429.1 yanaongeza ufanisi wa bandari hiyo kupakia na kupakua mizigo na kuifanya kuwa lango kuu la biashara kitaifa na kimataifa.

"Ni muda sahihi sasa kwa wafanyabiashara wa Mkoa wa Tanga na jirani kuchangamkia fursa zilizopo katika bandari hii," alisema Chatanda.

Makamu Mwenyekiti wa UWT, Zainab Khamis Shomari, alisema uchumi wa Tanga unakua kwa kasi kutoka na mradi huo wa kimkakati wa uboreshaji wa bandari hiyo.

"Ajira zimezalishwa kutokana na uboreshaji wa bandari hii ni wazi kuwa Rais Samia amedhamiria kutengeneza nafasi za ajira kwa makundi yote ya wananchi ndio maana sisi tumekuwa tukisema 2025 ni mitano tena Kwa Samia," alisema

# Chanzo cha maji chahujumiwa na watu wasiojulikana

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WATU wasiojulikana wanadaiwa kung'oa alama za mipaka 17 kati ya 25 zilizowekwa na serikali katika chanzo cha maji cha Isanja wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro.


Chanzo hicho cha maji kilichoko Kata ya Nasai, kimehujumiwa zaidi upande wa Kijiji cha Nrao.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watumia Maji wa Mto Sanya, Goodchance Moshi,waligundua hujuma hiyo baada ya kutembelea na kukagua chanzo hicho. "Wale wote waliong'oa bikoni (alama za mipaka) katika tindiga la Isanja, hatua kali dhidi yao zitachukuliwa ili iwe fundisho kwa wengine,"alisema.

Moshi ambaye pia ni Mjumbe wa Bodi Bonde la Pangani, alisema lazima hatua za kisheria dhidi yao zichukuliwe ili kuokoa chanzo hicho cha maji kugeuka kuwa jangwa. Moshi, alisema kabla ya kuweka alama hizo, waliwaita wananchi wanaozunguka eneo hilo na kuwaelimisha nia ya serikali.

"Lakini hivi karibuni tumepata taarifa za kushangaza kwa wasamaria wema kwamba zile alama zimeng'olewa.

...Sasa tunashangaa serikali inatenga maeneo kwa ajili ya vyanzo vya maji wananchi waweze kunufaika na maji, sasa watu wanakuja kung'oa tena," alisema.





# Kampeni dhidi ya malaria yazidi kupamba moto

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKOA wa Shinyanga unatarajia kupokea zaidi ya vyandarua milioni 1.5 kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa wa malaria kwa wakazi wake.

Takwimu hizo zilitolewa juzi mjini hapa na Ofisa Mradi wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria, Wilfred Mwafungo katika kikao cha maandalizi ya kampeni ya ugawaji wa vyandarua ngazi ya kaya inayotarajiwa kuanza nchini Januari 16, mwakani.

Mwafungo, alisema vyandarua hivyo 1,542,836 vitatolewa kwa mkoa huo na kugawiwa bure kwa wakazi wake kwa ajili ya kujikinga na mbu wanaosambaza ugonjwa wa malaria.

Alisema kati ya vyandarua hivyo 841,503 vitatolewa kwa Wilaya ya Kahama, Msalala 260,350, Ushetu 268,872 na Kahama 312,836.

Mwafungo alifafanua kuwa ugawaji wa vyandarua hivyo kwa wananchi unakuja kufuatia viashiria vya malaria mwaka 2022 kiwango cha kitaifa kuonyesha maambukizi yake nchini ni asilimia 8.1.

**Mboni, alisema awali baadhi ya viongozi hao walikuwa wakilalamikiwa kwa kushiriki kuuza na kubadilisha matumizi ya vyandarua hivyo na kukwamisha jitihada za serikali za mapambano dhidi ya malaria**

Alisema viashiria hivyo vinaonesha kuwa Tabora ambao ni miongoni mwa mikoa ya kanda ya ziwa unaongoza nchini kwa maambukizi kwa asilimia 23.4 ukifuatiwa na Mara asilimia 20 na Shinyanga asilimia 16.

"Ndio sababu ya serikali kutoa vyandarua bure kwa kila kaya nchini ili kupambana na ugonjwa huo wa malaria," alisema.

Mdhibiti wa Wadudu Dhurufu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Best Yoram aliwataka wananchi kuacha kutumia dawa bila kupima hospitalini ili kuondoa usugu wa vimelea vya vidudu vinavyosababisha malaria.

Yolam, alisema kuna dhana potofu imejengeka kwa baadhi ya watu ambao wakiumwa kichwa, wanahusisha kuwa ni moja ya dalili ya ugonjwa na kuanza kutumia dozi jambo ambalo ni hatari kiafya.

Awali akizungumza katika kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita aliwaonya watendaji kata, vijiji na wenyeviti wa serikali za mitaa na vijiji kujiepusha na uuzaji wa vyandarua hivyo vinavyotolewa bure na serikali kwa wananchi kukabiliana na malaria.

Mboni, alisema awali baadhi ya viongozi hao walikuwa wakilalamikiwa kwa kushiriki kuuza na kubadilisha matumizi ya vyandarua hivyo na kukwamisha jitihada za serikali za mapambano dhidi ya malaria nchini.

Kampeni hiyo ni mwendelezo wa ambazo zimekuwa zikifanyika nchini kwa miaka kadhaa sasa kutokomeza malaria.

Alisema viongozi watakaobainika kuuza vyandarua hivyo na wafanyabiashara watakamatwa na kufikishwa mahakamani kwa kosa la kuihujumu serikali.

Alisema kinachotakiwa kwa sasa ni kuendelea kuwapatia elimu wananchi umuhimu wa matumizi sahihi ya vyandarua hivyo ili kudhibiti ugonjwa huo kwa asilimia 63 na usafi wa mazingira.

Aliwataka viongozi hao kusimamia ugawaji wa vyandarua hivyo na kuhakikisha havigeuzwi nyavu za kuvua samaki, wigo wa kufugia kuku na bata na biashara kwa wananchi.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wa kikao hicho, Shekhe wa Wilaya hiyo, Alhaji Omari Damka, alisema ili kudhibiti malaria, elimu inahitajika kuendelea kutolewa zaidi kwa wananchi ili kutimiza dhamira ya serikali.

" Sasa ni msimu wa kilimo, wakulima wawapelekee vyandarua kupitia vyama vyao ili kuwafikia wengi zaidi," alisema na kuahidi kuendelea kutoa elimu.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha (kulia) akipokea vifaa vya ufundi ambavyo watakabidhiwa mabinti kwa ajili ya kupata ujuzi, ili wasijiingize kwenye vitendo vya ngono na kupata maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Kushoto ni Kaimu Meneja wa Mradi wa EPIC Getrude Saleko kutoka shirika la FHI 360. **PICHA: MARCO MADUHU**

# BoT yaja kidijiti kwa wateja

**Na Remmy Moka,** MWANZA

BENKI Kuu Tanzania (BoT), inatarajia kufanya majaribio ya mfumo wa kidijiti kushughulikia malalamiko ya wateja na wahudumu wa huduma za fedha ili kuendana na kasi ya maendeleo ya teknolojia duniani.

Mpango huo ulitangazwa juzi jijini hapa na Mkurungezi wa BoT Tawi la Mwanza, Gloria Mwaisambo wakati wa mafunzo ya matumizi ya mfumo huo unaotarajiwa kuanza kutumika Januari, mwakani.

Grolia, alisema kuwa mfumo huo utaondoa utaratibu wa sasa wa wateja kujaza taarifa zao za kibenki kwa njia ya makaratasi na kuwaondolea adha ya kutumia muda mrefu kufuata huduma za kifedha na kuwasilisha malalamiko yao katika taasisi husika kwa ajili ya utatuzi.

Alisema mfumo huo unatarajiwa kuongeza kasi ya kutatua malalamiko ya wateja na kutumia muda mfupi.

Grolia, alisema mfumo huo pia utatumika kutunza kumbukumbu tofauti na wa analojia ambao umekuwa ukitumika kwa muda mrefu.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo, akiwemo Meneja wa Huduma kwa Wateja wa Benki ya Afrika Tanzania (BOAT), Baraka Mwakaje, alisema mfumo wa awali ulikuwa ukichelewesha kutatua changamoto za wateja na kutohifadhi kumbukumbu.

Mwakaje, alisema kujaza taarifa kwa njia ya mtandao kutarahisisha kutoa huduma kwa wateja na kushughulikia changamoto zinazojitokeza haraka.

# Wenyeviti marufuku kujipatia rushwa kwa mihuri ya ofisi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Annamringi Macha amewapiga marufuku wenyeviti wa vijiji, vitongoji na mitaa mkoani hapa kutumia mihuri ya ofisi kujipatia rushwa kwa wananchi na kuonya watakaokiuka watachukuliwa hatua.

Macha alitoa onyo hilo juzi wakati akifungua mafunzo ya uongozi kwa wenyeviti hao wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ya kuwapa ujuzi juu ya utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema baadhi ya viongozi waliochaguliwa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika Novemba 27, mwaka huu ni wapya, hivyo wanatakiwa kuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao kwa wananchi na siyo kuendekeza rushwa.

"Nawapongeza kwanza kwa kuchaguliwa na wananchi, nendeni mkawe wazalendo na waadilifu katika kuwatumikia wananchi, " alisema na kusisitiza kuwa: Msitumie mihuri vibaya kwa kuendekeza rushwa na kujipatia mapato ambayo yasiyo halali." Macha, aliwasihi kuepuka kuwa chanzo cha migogoro ya ardhi katika maeneo yao kwa kuidhinisha nyaraka bila ya kujiridhisha kuwa eneo husika halina mgogoro.

Alisema wanatakiwa kuhakikisha kama kuna mtu ameuziwa eneo lenye mgogoro na kuepuka kuwa chanzo cha kuchochea mgogoro huo.

Baadhi ya viongozi hao akiwamo Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kasubuya (CHADEMA), Juma Tungu, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kuwatumikia wananchi. Ofisa Uchaguzi wa Halmashauri hiyo, Oscar Lupavila, alisema mafunzo hayo yatawasaidia viongozi hao kuwatumikia kwa wananchi na kuwaletea maendeleo.




Tabasamu ya wakulima chai kupata masoko Japani na uarabuni, ifike mazao mengine

BUFE

IJUMAA DESEMBA 20, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




# Simulizi wachimbaji wadogo kugeuka waajiri, watetezi wa wenzao serikalini

## • Mmoja kawachukua wenzake 100, mfadhili huduma

**Na Ibrahim Yassin, Chunya**

UNAPOZURU wilayani Chunya mkoani Mbeya, kuna mchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu katika halmashauri ya wilaya hiyo, kazi yake mpya inatoa ajira kwa vijana zaidi ya 100.

Waajiri hao ni kutoka mikoa mbalimbali, huku akitoa mapendekezo kwa serikali namna ya kuongeza tija ya uzalishaji ikiwamo, kuondoa changamoto zilizopo kwa wachimbaji.

Hiyo inatokea, huku sekta ya madini ikiwa moja ya vyanzo muhimu vinavyoingizia mapato makubwa umma, huku serikali nayo ikitegemea mapato kutokana na tozo za kodi kutoka katika sekta hiyo.

Wakati serikali ikiweka mikakati yake kuongeza mapato na kuingiza maboresho kwa wachimbaji, inayojumuisha kuwapatia mikopo, pamoja na maeneo sahihi ya uchimbaji, kuna utata unajitokeza katika mchakato kamili wa kufanikisha kazi hiyo.

Hiyo inatajwa kwa sasa inawafanya wengi wamekuwa wakichimba kwenye maeneo yenye leseni za watu licha ya kuwa maeneo hayo hawayatumii.

Akizungumza na Nipashe, mbunifu Khamis Rajab Salum, ambaye ni Mkurugenzi wa kampuni yake, anasema alikuwa mjasiriamali anayefanya kazi ya kuchomelea vyuma, baadae akajiingiza kwenye uchimbaji madini, alikotumikia kwa miaka saba, hata kufanikiwa kuajiri vijana zaidi ya 100 wa kada mbalimbali, mgongo wa kampuni yake.



Mchimba madini mdogo, Khamis Rajab Salum, aliyeibuka hata kuwaajiri wenzake 100,akiwa kwenye mradi wake **PICHA:IBRAHIM YASSIN.**

Anasema, hadi sasa anamiliki migodi mitatu ya kisasa, ikiwa ngazi ya juu zilizoko wilayani Songwe na mbili, huko Makongolosi, Chunya, huku akiwa na mtambo mkubwa maarufu 'karasha' za usaga mawe tani tatu na nusu kwa saa.

Salum anasema, katika jitihada zake anamiliki malori manne, vilevile trekta, mitungi na mitambo ya kuchoma umeme.

Anajigamba ni hali inayomfanya kulipa kodi na mishahara ya wafanyakazi wake kwa wakati, huku akishiriki kikamilifu kwenye shughuli za kijamii katika maeneo na nje ya miradi wake.

Salum anaeleza sehemu ya faida anayopata amekuwa akitoa misaada kwa watoto yatima kwenye vituo vilivyopo mkoani Mbeya, akirejea mfano wa hivi karibuni amechangia mifuko 100 ya saruji yenye thamani ya shilingi milioni 2.1 kwenye ujenzi wa Kituo cha Afya Makongolosi.

Pia anasema, michango anaielekeza kwenye nyumba za ibada, wazee wasiojiweza jijini Mbeya na kwenye ujenzi wa shule ya sekondari, akinena nako katoa mifuko 100 ya saruji.

**MAONI YAKE KISERIKALI**

Mchimbaji huyo mdogo, anaitaja sekta hiyo ya madini ni muhimu na inachangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa, hivyo ili mafanikio makubwa zaidi yapatikane, serikali kupitia Wizara ya Madini, iwape maeneo maalum ya kuchimba wachimbaji wadogo na kuwapatia mikopo.

Anasema, wachimbaji wadogo wengi hawana migodi, wengi wao zaidi ya 200 walikuwa wakichimba kwenye eneo linalojulikana kwa jina la 'Gepu' lakini akajitokeza mtu aliyewafukuza akidai eneo hilo ni lake na amepewa leseni.

Kufukuzwa kwa wachimbaji hao, anakutaja kumewapa magumu anaowataja kuwa 'wachimbaji wenzake', kwamba wamehamia kwenye eneo lake kufanya kazi yao.

Anasema, hadi sasa kuna maeneo (makarasha) zaidi ya 14 yamefungwa na kila moja linakuwa na wachimbaji kati ya 10 hadi 12 wanaofanya kazi hapo.

"Wachimbaji hawa wamefukuzwa kwenye eneo lile la 'gepu', wamekuja kuchimba kwenye eneo langu na wamefunga makarasha.

"Siwezi kuwafukuza kwa kuwa wanatafuta riziki ila inatakiwa serikali itafute eneo lingine lisilotumika kuwahamishia wachimbaji hawa ili kuepuka kutofanyika

Inaendelea Uk 14

## UCHUMI

TAKUKURU WAJA NA LAO...

# Mipango na ufanisi wa nguvukazi, inaingiziwa elimu rushwa kuanzia ngazi ya shule, vyuoni

## •Ushuhuda; mijadala na vilabu Dodoma, waonesha njia...

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma imekuwa na utaratibu wa kuandaa midahalo mbalimbali inayohusisha wanafunzi wa vyuo vikuu, sekondari na shule za msingi.

Hapo mtazamo ni kupanua wigo wa uelewa kwa jamii kuhusu madhara ya kutoa rushwa au kupokea mahali pa kazi, vyuoni na kwingineko.

Mwezi uliopita, TAKUKURU mkoani Dodoma, kwa kushirikiana na wadau, ikiwamo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, pia Mamlaka ya

1. Kupambana na Dawa za Kulevya, wakaandaa mdahalo uliohusisha vyuo vya Elimu ya Juu na kati, ukilenga kuwapa elimu Wanafunzi, jamii na makundi tofauti walioalikwa.

Mada mojawapo ilijadili kukosekana uzalendo, kunavyomnyima raia haki ya msingi ya kufanya uamuzi sahihi kwenye, kitendo ambacho TAKUKURU ilidhamiria kuwekwa mikakati ya kuhakikisha elimu inafikia kupata uelewa unaohusu suala hilo.

Baadhi ya vyuo vilivyoleta washiriki kwenye mdahalo huo, ni wasomi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Chuo cha Mipango na Maendeleo yaVijijini (IRDP), Chuo cha Serikali za Mitaa na Chuo cha Ufundi VETA.

Hapo wamekuwa wakibadilishana hoja kuhusu rushwa inavyoathiri miradi ya maendeleo, taasisi, pia mtu mmoja mmoja.

Katika majibizano yao kwa hoja za msingi, yalizidi kuongeza wigo wa uelewa wa madhara ya rushwa, huku jamii ikijitokeza kushuhudia mdahalo huo, lengo kuu ilikuwa ni kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kuelewa juu ya madhara ya utoaji rushwa kwa jamii inayotuzunguka.

Hilo limeifanya taasisi hiyo kuanzisha klabu za kupinga rushwa ngazi ya vyuo vikuu, kati, shule za msingi na sekondari mkoani Dodoma, hata kutumika kuwa mabalozi wa kusaidia

kupiga vita rushwa, pamoja na kuielimisha jamii katika maeneo wanayotoka.

Taasisi ya rushwa mkoani hapa, kwa kushirikiana na walimu wa shule hizo, kupitia maofisa wa TAKUKURU, wamekuwa wakitoa elimu kwa klabu husika, ili kuwajengea uwezo wanafunzi wanaounda

klabu, kuwa mabalozi wazuri wa kuelimisha katika maeneo wanayotoka, pindi watakapohitimu.

Hilo limetokana na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa, ikielezwa shuleni kupinga rushwa kutoa upinzani mkubwa katika midahalo inayohusu kupiga vita rushwa, chini ya usimamizi wa taasisi hiyo wanapoalikwa kushiriki.

Maofisa wa TAKUKURU, katika hatua yao wanatanua wigo wa elimu hiyo katika maeneo mbalimbali mikoani kwa kushirikiana na walimu wa klabu katika shule na vyuo mbalimbali ambazo hazijaundwa.



Wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu na kati mjini Dodoma, wakifuatilia mdahalo kuhusu vita ya rushwa. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

### MKUU TAKUKURU MKOANI

Victor Swella, anasema siri ya mafanikio kwenye vita hivyo dhidi ya rushwa, ni kutolewa elimu kwa wenye rika hizo, ili kuwajengea uwezo tangu awali ya kukataa vitendo vya rushwa, popote penye viashiria vya aina hiyo.

Swella anasema, uanzishwaji klabu hizo ni pamoja na kuhitaji kupanua wigo wa utoaji elimu kwa jamii, kuhusu vita vya rushwa, huku ikiwaandaa kuwa mabalozi wa kupiga vita rushwa sehemu zao baadae katika maeneo watakayokuwa pindi watahitimu masomo yao.

Swella anasema: "Tunahitaji kuona elimu ya kupiga vita rushwa inaenea katika maeneo

mbalimbali ndio maana unaona tumeshirikiana na baadhi ya vyuo vikuu, vya kati pamoja na shule za msingi na sekondari.

Anaendelea: "Ili kuhakikisha elimuya kupiga vita rushwa pamoja na madhara yake inaenea kwa kiasi kikubwa."

Kwa mujibu wa Swella, TAKUKURU mkoani Dodoma, imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu tafsiri pana ya vita vya rushwa, akitaja vinachangia kwa kiasi kikubwa kudhoofisha miradi ya maendeleo ya kimkakati serikalini.

Anafafanua kuwa, katika utekelezaji jukumu la kutoa elimu, wamewafikia wananchi takribani 78,896 kwa njia ya mikutano ya hadhara katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Dodoma.

Lingine, anataja mafanikio ya utoaji elimu kwa njia ya maonesho yaliyolenga elimu ya madhara ya rushwa, ifanikiwe akiwa na ufafanuzi kwamba:

"Kuna klabu 670 za wapinga rushwa ambazo zipo vyuoni, sekondari, pamoja na shule za msingi.

"Ni klabu zinatengeneza mabalozi wazuri katika utoaji elimu kwenye maeneo wanayotoka na kwenye hili, tumezidi kupanua wigo wa utoaji elimu ya madhara ya rushwa,"anasema Swella.

### MWENYEKITI MIDAHALO

Mwenyekiti wa Midahalo ya TAKUKURU, Dodoma mjini, Francis Magoha, anasema midahalo ya TAKUKURU huandaliwa kwa ushitrikiano na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, imekuwa kivutio kwa wanafunzi kujiunga na vilabu vya rushwa vyuoni na shuleni.

Magoha anasema, TAKUKURU imekuwa ikiendesha midahalo kwa nyakati tofauti, ikizihusisha shule na vyuo vya ngazi tofauti, kukiwapo mada zinazohamasisha madhara ya rushwa kwenye mikusanyiko.

Anaisifu kuwa, imesaidia kutoa elimu kwa wanafunzi, katika mtazamo mpana wa kupiga vita rushwa katika maeneo mbalimbali, ikiwamo masomoni kwa tafsiri "rushwa kwa mtu yeyote hairuhusiwi."

Magoha anataja hali ya midahalo hiyo, imekuwa ikifanyika kila mwaka kwa kuwakutanisha wanavyuo wa elimu ya juu na kati, huwa wanajibazana kwa hoja lengo ni kuona namna wanapata uelewa kuhusu suala zima la kupiga vita rushwa.

### WASHIRIKI WANENA

Sauda Mahamudu, kutoka chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), anasema elimu ya kupiga vita rushwa isiishie kwa wanafunzi, bali kumfikia kila mwananchi kuyajua mapambano dhidi ya rushwa si ya mtu mmoja mmoja, bali ya wote.

"Elimu hii isiishie kwa wanafunzitu bali ifike hadi pembezoni ili kuhakikisha wananchi wanaelewa madhara ya utoaji rushwa mahali pa kazi sio jambo sahihi," anasema Mahamudu.

Mshiriki Ibrahimu Kayonko, anasema elimu inapaswa kutolewa zaidi pembezoni, ili kuwasaidia wananchi kuelewa madhara ya utoaji na kupokea rushwa katika maeneo mbalimbali.

Anasema kuanzishwa vilabu vya kupinga rushwa katika vyuo na shule za msingi na sekondari, imewasaidia wanafunzi kupata uwelewa zaidi ya madhara ya rushwa kwa mtu anayetoa na anayepokea.

### DC DODOMA MJINI

Jabiri Shekimweri ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, anaipongeza TAKUKURU Dodoma kwa kuendeleza wigo wa utoaji elimu ya kupinga rushwa katika maeneo mbalimbali mkoani humo.

Anasema, ni hali inayozidi kuonesha nia ya kuungana na serikali katika mapambano dhidi ya rushwa.

Shekimweri anasema, ubunifu wa kuanzisha klabu za kupinga rushwa vyuoni na shuleni ni jambo zuri, kwa sababu wameanza kutengeneza mabalozi wa

kupiga vita rushwa kutoka wakiwa elimu ya msingi, jambo analolisifu kuwa zuri ndani ya jamii inayowazunguka.

"Hii imesaidia kuongeza wigo wa utoaji elimu kwa jamii, lakini kushawishi watu wajiunge kwenye klabu za wapinga rushwa,"anasema Shekimweri.

Anafafanua kuwa, elimu ya madhara ya kupokea na kutoa rushwa, inapaswa kuzingatiwa, kwa sababu watu wasipokuwa na elimu ya rushwa, itawawia vigumu kujua madhara yanayotokea pale mtu anapotoa rushwa au kupokea rushwa ili afanikishe suala lake.

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tabasamu la wakulima chai kupata masoko Japani na Uarabuni, ifikie mazao mengine






NA HALFANI CHUSI

ZAO la Chai ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi nchini. Linaongeza ajira na pato la mtu mmoja mmoja.

Kwa miaka kadhaa wakulima wa zao hilo, wamekuwa wakipitia wakati mgumu kupata masoko ya uhakika jambo ambalo liliwakatisha tamaa baadhi yao.

Hata hivyo, kwa sasa pasina shaka juhudi za kiserikali zimejikita katika kutatua tatizo hilo. Jitihada kubwa imeelekezwa katika kutafuta masoko mapya na kurejesha yaliyopotea.

Hivi karibuni, bodi yenye mamlaka na zao hilo, imerejesha soko la chai la nchini Oman na Sudani na sasa uongozi wake umekwenda nchi za Saudi Arabia kwa lengo la kuongeza soko la bidhaa hiyo katika nchi za Kiarabu.

Kwanini Uarabuni? Hiyo inatokana na desturi za watu wengi kutoka nchi hizo, kupenda kinywaji hicho.

Ni jitihada zinazoacha tabasamu kwa wakulima pale wanaposikia mipango na jitihada wanapiganiwa zao lao kumea.

Jingine kubwa, ni kile kitendo cha kuwaleta nchini wataalamu wa chai kutoka Japan, waliotembelea mashamba yaliyoko katika mikoa ya Njombe na Iringa na baadhi ya viwanda vinavyochakata chai kwa lengo la kujifunza fursa zilizopo na kubadilishana uzoefu katika zao hilo.

Hata hivyo, walionesha kuipenda chai ya Tanzania wakiisifu ni nzuri kutengeneza kinywaji cha kijani, ambayo nchini kwao imeshika soko.

Jitihada hizo, ni mpango madhubuti wa serikali katika kuinua sekta ya chai na wakulima wake na hata kumaliza vilio vyao vya kila siku vya kukosa soko.

Kutokana na ujio wa Wajapani, kunafafanuliwa kwamba matarajio yao baada ya ugeni huo ni mapinduzi ya viwanda na kuongeza ubora wa chai, ili iwe rahisi kulikamata soko la ndani na nje ya nchi.

Sambamba na juhudi hizo, pia serikali inaendelea na mpango wake wa kushawishi wawekezaji kuwekeza katika sekta kwa kujenga viwanda na kulima mashamba makubwa.

Katika ufafanuzi wake, chombo chenye mamlaka na zao hilo, kinasema hali ya soko inazidi kuwa nzuri na hata maeneo waliyokwenda wameonesha kuikubali chai ya Tanzania.

Selemani Chillo, ofisa wa kiserikali mwenye dhamana hiyo anatamka: "Tunaendelea na juhudi za kushawishi na kuitangaza chai yetu nje ya mipaka ya Tanzania, kushawishi wawekezaji tunaamini tukifanikiwa katika hilo thamani ya zao hilo itakuwa juu na watu wataipenda chai ya Tanzania."

Kwa kifupi, ipo mipango mingi inayoratibiwa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, ikiwamo kufanya uwekezaji utakaoendana na teknolojia ya kisasa, mkakati wa kuweka viwanda vidogo viodogo katika mashamba ya wakulima, utanuzi wa masoko, pamoja na kuvuta wawekezaji kutoka nchi za nje.

Ofisa Kilimo Idara ya Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo, Bahati Majaliwa, anasema mpango wa serikali ni kujenga viwanda vidogo vidogo vitakavyo wasaidia wakulima kusindika chai ili waweze kupata faida zaidi kutokana na mauzo.

"Wajapan wameipenda sana chai yenye majani membamba, na inazalishwa kwa wingi, katika maeneo mengi ya uzalishaji hapa nchini ikiwamo yale ya mkonge lakini nchini kwetu ni zaidi ya asilimia 80 ya chai hiyo inazalishwa.

"Wakulima waendelee kutunza mashamba yao vizuri ili kupata tija kutokana na majani watakayozalisha" anasema Majaliwa aliyekuwa miongoni wa walioongozana na ugeni huo kutoka Wizara ya Kilimo

Majaliwa anasema mkakati wa Wizara ya Kilimo kwa sasa ni kuhakikisha wakulima wanasindika chai yao na kwamba mpango uliopo ni kuwekeza katika viwanda vya wakulima wadogo.

"Bado Wizara ina nia ya kuhakikisha uwekezaji viwanda unafanyika ili wakulima waweze kusindika chai.

"Wakulima wa chai watambue serikali inaendelea na jitihada kuhakikisha zao la chai linaendelea hapa nchini kwa kuweka viwanda vya wakulima wadogo" anasisitiza.

Anasema ujenzi wa viwanda kwa wakulima wadogo utasaidia kuwainua kiuchumi na kuzalisha chai yenye tija itakayoleta ushindani katika soko la kitaifa na kimataifa.

UCHUMI

# ZIFAHAMU FAMILIA TAJIRI DUNIANI

Katika orodha ya kila mwaka ya familia tajiri zaidi ulimwenguni ambayo huandaliwa na Bloomberg, familia ya Walton, mmiliki wa maduka makubwa nchini Marekani Walmart, ilishika nafasi ya kwanza mnamo 2024.

Miongo sita baada ya Sam Walton kufungua duka kuu la kwanza huko Arkansas, warithi wake ni matajiri zaidi kuliko hapo awali kutokana na utendaji uliovutia wawekezaji wa hisa za kimataifa, ambazo thamani yake imeongezeka kwa asilimia 80 mwaka huu.

Siri mojawapo ni kampuni zinazounda orodha hiyo, kwa mujibu wa Bloomberg, ni kwamba zimeendelea kuwa na umoja katika umiliki wa mali zao na, wakati fulani, zimeunda makubaliano ya kibiashara ambayo yanasimamia kuunganisha utajiri wao.

Familia nyingi katika orodha ya mwaka huu, kwa mujibu wa Bloomberg, zimekuwa tajiri zaidi kutokana na faida kubwa iliyorekodiwa kwenye soko la hisa.



Rob, Alice na Jim Walton walirithi utajiri wa muasisi wa Walmar, Marekani. **PICHA: MTANDAO.**

**FAMILIA TAJIRI DUNIANI**

**1. Familia ya Walton;**

**Utajiri wake Ni Dola za Marekani bilioni432** .Walton wanamiliki takriban 46% ya maduka makubwa, hisa ambayo ni msingi wa utajiri mkubwa wa familia hiyo.

Mwanzilishi wake, Sam Walton, aligawanya mali kati ya watoto wake kimkakati ili kuimarisha uchumi wa familia.

**2. Familia ya Al Nahyan:**

**Wana Dola za Marekani bilioni 323,**

Katika Umoja wa Falme za Kiarabu, familia tawala ya Al Nahyan ilizalisha utajiri wake kutokana na biashara ya mafuta.

Mtawala wa Abu Dhabi (mmoja kati ya wafalme saba), Shekhe Mohammed bin Zayed Al Nahyan, pia ni rais wa nchi hiyo.

**3. Familia ya Al Thani: Utajiri wao Dola 172 bilioni na wanaishi Qatar.**

Serikali ya familia ya Al Thani nchini Qatar ina maslahi ya kibiashara katika sekta ya mafuta na gesi.

Wanafamilia wanashikilia nyadhifa maarufu za kisiasa na wanamiliki kampuni kubwa katika tasnia mbalimbali.

Familia ni kubwa, ingawa nguvu yake kiuchumi imejilimbikizia katika maeneo machache muhimu.

**4. Familia ya Hermes:**

**Pesa zao ni Dola za Marekani 170** bilioni na wanaishi Ufaransa, wanamiliki kampuni ya mitindo ya kifahari nchini Ufaransa.Miongoni mwa wanafamilia wanaoshikilia nyadhifa za utendaji katika kampuni hiyo ni Axel Dumas, Mkurugenzi Mtendaji.

**5. Familia ya Kochs: P**

**Utajiri wao Dola bilioni 148.** Ndugu Frederick, Charles, David na William Koch walirithi kampuni ya mafuta kutoka kwa baba yao, Fred. Lakini baada ya msuguanoo, ni Charles na David pekee waliobaki kwenye biashara hiyo.

Kampuni ya Koch ina biashara katika mafuta ya petroli, kemikali, nishati, madini, teknolojia ya komputa, fedha, biashara ya bidhaa, uwekezaji, miongoni mwa nyingine.

**6. Familia ya Al Saud:** Mwanamfalme wa Saudi Arabia Mohammed bin Salman ni sehemu ya familia. Sekta yao ni viwanda wakiwa na utajiri wao Dola za Marekani bilioni 850.

Utajiri wa familia ya Kifalme wa Saudia,

**7. Familia ya Mars: Utajiri wao ni Dola bilioni 133,** wakimiliki kampuni ya Mars inayojulikana kwa bidhaa zake kama vile biskuti za chokoleti maarufu, ingawa bidhaa za utunzaji wa wanyama sasa zinachangia zaidi ya nusu ya mapato ya kampuni hiyo.

**8. Familia ya Ambani:**

Wana kampuni ya Reliance Industries

yenye utajiri wa Dola bilioni 99 nchini

India. Mukesh Ambani ndiye anayesimamia eneo kubwa zaidi la kusafisha mafuta duniani.

Anaishi katika jumba la ghorofa 27 huko Mumbai, linalotajwa kuwa makazi binafsi ya gharama kubwa zaidi ulimwenguni. Yeye na kaka yake walirithi mali kutoka kwa baba yao.

Familia hiyo iliangaziwa hivi karibuni katika harusi ya Mukesh Ambani na Radhika Merchant. Ndoa hiyo ilitanguliwa na miezi minne ya matukio ya kifahari, ikiwa ni pamoja na matamasha ya nyota wa pop kama Rihanna.

**9. Familia ya Wertheimer: Utajiri: Dola za Marekani bilioni 88** nchini Ufaransa na wanandugu Alain na Gerard Wertheimer walirithi utajiri ambao babu yao aliyebuni ufadhili Coco Chanel huko Paris katika miaka ya 1920.

Familia yake inamiliki jumba la mitindo na pia farasi wa mashindano na mashamba ya mizabibu.

**10. Familia ya Thomson: o chpi Utajiri: Dola za Marekani bilioni 87** huko nchini Canada.Familia inamiliki takriban 70% ya hisa katika data na huduma za kifedha kutoka Thomson Reuters.

Utajiri wa familia tajiri zaidi ya Canada ulianza mapema miaka ya 1930 wakati Roy Thomson alifungua kituo cha redio huko Ontario.

- *Kwa mujibu wa BBC.*

## SIMULIZI WACHIMBAJI WADOGO KUGEUKA WAAJIRI, WATETEZI WA WENZAO SERIKALINI

Inatoka Uk 11

kwa mambo mabaya ikiwaemo wizi,"anasema.

Khamis anashauri serikali kutambua kuwa wachimbaji wasio na maeneo, ndio wazalishaji wakubwa wa dhahabu nchini, kwani wanapoingia kujipatia riziki, huongeza wingi wa dhahabu kitaifa kwa ujumla.

Anaongeza kuwa, hata Ofisi ya Madini mkoani humo imeshamtunuku tuzo mara nyingi.

**MCHIMBAJI ALIYEUIBUKA**

Zebedayo Mumusi, ambaye ni mchimbaji mdogo, anasema hali ya kuwapo vitalu vya uchimbaji ambavyo wenyewe hawafahamiki, umekuwa ukiwakwaza wengi.

Hapo anafafanua: "Tunasikia kuwa kuna vitalu vimepatikana, lakini serikali inapaswa kutangaza au kuitisha mkutano kwenye maeneo husika, ili kila mmoja asikie na kama atapenda kupata eneo lake basi iwe ni suala la kuomba lakini wakiwa wame fahamishwa."

Anaendelea kushauri kuwa serikali kwa kutumia mbinu ya kusaidia vijana wasiomudu gharama, wapatiwe kama vikundi, ili kuwawezesha kuzalisha dhahabu, bidhaa yenye nafasi kubwa katika pato la taifa.

Mumusi anasema kuwa, elimu zaidi kwa wachimbaji ifanyike ikiwamo ya kisheria, kwani migogoro imekuwa ikijitokeza ya wachimbaji na wenye maeneo, sehemu nyingi zikiwa zimetelekezwa na serikali inakosa mapato.

Hapo anamaanisha dhana ya elimu kwa wauzaji baruti, ifanyike kwa wanaoziuza kienyeji.

Mchimbaji mkongwe, George Kasanda, ambaye kwa sasa anamiliki mgodi na akiwa na wafanyakazi zaidi ya 50, anatumia uchimbaji wa mashine zaidi.

Anataja wakati Waziri wa Madini, anamtaja Profesa Sospeter Muhongo, anamsifu kuwatetea sana wachimbaji wadogo.

Anasema zama za miaka 2010, kukiwapo Waziri huyo, binafsi ana kumbukumbu jinsi wachimbaji wadogo walivyoshiriki kuandaa Sera ya Madini, akiwamo yeye mwenyewe.

Anasema, ili kuondoa migogoro kati ya wataalamu wa wakulima na wachimbaji, ni muhimu wakaletwa waaalamu madini na wahusika wengine kutoa elimu ya uhalisia na mipaka iliyoko kwenye maeneo hayo ya uchimbaji, kilimo na makazi.

Kasanda anashauri hapo kuwa, maeneo yenye mikondo ya madini, hayafai kuwe makazi ya watu na wanapaswa kuandaa ramani husika, serikali ikiruhusu watafiti binafsi, ili kuongeza ushindani unaikuza sekta hiyo.

Aidha, Kasanda anashauri kuwa serikali itafute mitambo ya utafiti na ikiwezekana iwakodishie wachimbaji wadogo, ili kuendana na teknolojia ya kisasa.

Hadi sasa anataka wachimbaji wengi wanatumia nyenzo za kizamani, inayochelewesha upatikanaji dhahabu kwa wingi.

**UONGOZI WILAYA**

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa Mbeya, Laurent Mayala, anasema serikali imejipanga kuhakikisha wachimbaji wanaondolewa changamoto zao ikiwa.

Hapo anataja kujumuisha kupatiwa maeneo ambapo tayari zaidi ya vitalu vyenye leseni 1500 vilivyokuwa havitumiki, huku mambo mengine yakiendelea kutatuliwa.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mbaraka Batenga, anasema kutokana na sekta hiyo ya madini kuwa umuhimu, serikali imejipanga kuwaongezea tija wachimbaji na kuweka lengo la kukusanya kilo 500 kila mwezi.

Katika hilo anataka kufanikishwa vitalu vyenye leseni 1505 vilivyokuwa havitumiki vimechukuliwa na kupewa wachimbaji wadogo kwa kuanzia.

Mkuu wa Wilaya anasema,uongozi wake unaendelea kuzishawishi benki ziwakopesha wachimbaji wadogo, kwa ajili ya kufanikisha shughuli za uchimbaji. Anakiri kutambua umuhimu wa wachimbaji wadogo, akisema kuwa 'ni benki ikawaamini.'

Pia, Batenga anasema hakuna mchimbaji mwenye lesseni amelalamika kushindwa kurudisha deni, hivyo ana matumaini hata benki hizo zikiwakopesha, deni kulipwa kwa mujibu wa makubaliano.



# Wafanyabiashara wa pembejeo njia panda

**Na Renatha Msungu**
DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe ametoa mwaka mmoja kwa wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo kujiendeleza kielimu, lasivyo hawataruhusiwa kutoa huduma kwa wakulima nchini.

Bashe alitoa kauli hiyo jijini hapa katika mkutano wa wadau wa mbegu ulioandaliwa na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania ( TOSCI).

Alisema ametoa kipindi hicho ili wafanyabiashara hao wakizi masharti ya uuzaji wa pembejeo lazima wawe wamesomea fani hiyo kuanzia ngazi ya cheti, diploma na shahada.

Alisema baada ya kukidhi kigezo hicho, wanaweze kutoa ushauri kwa wateja wao wa zana za kilimo katika maeneo mbalimbali nchini.

"Nawapa kipindi cha mpito cha mwaka mmoja kuhakikisha wafanyabiashara ambao hawana utaalam wa sekta hiyo kuhakikisha wanakwenda kusomea taaluma hiyo," alisema Bashe.

Alisema baada ya kipindi hicho, wataalamu wa wizara hiyo watafanya ukaguzi wa maduka ya pembejeo nchini kubaini kama wafanyabiashara hao wametimiza vigezo vinavyotakiwa kwa uuzaji wa pembejeo. Alisema wafanyabiashara ambao watabainika hawajajiendeleza kielimu, watakuwa wamekosa sifa ya kuendelea na biashara hiyo nchini.

**"Wamiliki wa maduka ya pembejeo hakikisheni mnatimiza vigezo mlivyotakiwa kuwa navyo, nahitaji kuona maduka hayo yanatoa huduma...**

Vilevile, Bashe alitoa siku saba kwa wamiliki wa maduka ya pembejeo yaliyofungwa na wakaguzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu nchini (TOSCI) kwa kukosa vigezo, wahakikishe wanaondoa dosari hizo na kuruhusiwa kuendelea kutoa huduma kwa wateja wao kwa msimu huu wa kilimo.

"Wamiliki wa maduka ya pembejeo hakikisheni mnatimiza vigezo mlivyotakiwa kuwa navyo, nahitaji kuona maduka hayo yanatoa huduma hususani kuelekea msimu wa kilimo," alisema Bashe. Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngwediagi, alisema taasisi hiyo itaendelea kusimamia uzalishaji bora wa mbegu katika ngazi ya wakala na mifumo ya usambazaji ili kuhakikisha wakulima wanaongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na kuinua uchumi wao na familia zao.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea nchini (TFRA), Joel Lawrence, aliusifia mfumo wa kidijiti wa ununuzi na usambazaji wa pembejeo kuwa umewawezesha wakulima zaidi ya milioni nne kujisajili.

Lawrence, alisema hakuna mkulima atakayenunua pembejeo bila ya kuandikishwa kwenye mifumo ya kidijiti ambayo imetolewa na serikali. Aliwataka wakulima kuchangamkia fursa zinazotolewa na serikali ili waweze kuongeza uzalishaji wa mazao na kipato.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu akifunga kikao kazi cha wakuu wa idara za utawala na usimamizi wa rasilimali watu kilichofanyika Jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wenyeviti wapewa angalizo

**Na Peter Mkwavila,**
CHAMWINO

MKUU wa Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Janeth Mayanja amewataka wenyeviti wapya wa vijiji na vitongoji kuepuka kuwa sehemu ya kuzalisha migogoro ya ardhi kwa kuuza maeneo ya umma na watu binafsi.

Mayanja alitoa wito huo juzi wakati akifungua mafunzo elekezi kwa viongozi hao wa vijiji vya Buigiri Mwegamile na Chinangali waliochaguliwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika nchini mwezi uliopita.

Alisema viongozi hao wanapaswa kutatua migogoro na sio kuzalisha migogoro hiyo na kusababisha kuendelea kukithiri katika maeneo yao.

Alieleza wananchi wamewachagua wakitegemea watashirikiana kuleta maendeleo pamoja, hivyo wanatakiwa kuwa waaminifu na kutoa haki bila ubaguzi wa dini, siasa, ukabila na rangi.

Diwani wa Kata ya Buigiri, Keneth Yindi, aliwaasa wenyeviti hao kutotumia nafasi zao kwa manufaa binafsi na kukwamisha malengo ya serikali kuwaletea wananchi maendeleo. "Msitumie nafasi zenu kuwa sehemu ya kutengeneza mianya ya kujipatia mali na fedha kwa njia za rushwa kutoka kwa wananchi ambao wenyewe ndio wamewapa ridhaa ya kuwaongoza," alisema.

Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Wilaya ya Chamwino, Lina Mazigo aliwakumbusha viongozi hao kusimamia sheria katika kutoa maamuzi na kuepukana na upendeleo ambao unashawishi kujipatia mali na fedha kwa njia isiyo halali.

# Mifugo kuanza kuchanjwa Januari kudhibiti magonjwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imepanga kutumia Sh. Bilioni 216 kutoa chanjo kwa kipindi cha miaka mitano ili kudhibiti magonjwa ya mifugo nchini kuanzia mwezi ujao.

Awamu ya kwanza itaanza Januari 2025 na kwamba kiasi cha Sh.Bilioni 28.1 kinatarajiwa kutumika kufanikisha mpango huo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Dk. Ashatu Kijaji, alitangaza mpango huo juzi jijini hapa wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Chanjo za Mifugo Kitaifa.

Kijaji, alisema serikali imeridhia kugharamia mpango wa chanjo hiyo kuanzia mwaka huu hadi 2029.

"Katika mwaka wa fedha 2024/25 serikali imetenga Sh.bilioni 28.1 kuchanja ng'ombe dhidi ya homa ya mapafu, ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na mdondo wa kuku ili kuwasaidia wafugaji wetu kote nchini," alisema.

Alisema awamu ya kwanza, Serikali itachanja ng'ombe 19,097,223, mbuzi na kondoo 20,900,000 na kuku wa asili 40,000,000.

Kijaji, alisema lengo la serikali ni kutoa chanjo kwa mifugo angalau asilimia 70 ya idadi ya mifugo husika kwa miaka mitano mfululizo.

"Kwa sasa hali ya uchanjaji kwa ng'ombe, Mbuzi na Kondoo ni asilimia 21, kuku wa kienyeji asilimia 40 na kuku wa kisasa ni asilimia 100."

"Hivyo kampeni hii itasaidia kutokomeza magonjwa ya mifugo, kutoa ajira za muda mfupi kwa vijana na wanawake 3540 na kuongeza usafirishaji wa nyama nje ya nchi kutoka asilimia 14 ya sasa na kufikia asilimia 30 ifikapo mwaka 2029," alisema.

Alisema katika kufanikisha kampeni hiyo nchini, serikali itachangia nusu bei ya gharama za chanjo ili kuwarahisishia wafugaji kuchanja mifugo yao.

"Rais Samia Suluhu Hassan ameahidi kuwa serikali itachangia nusu ya bei kwa ajili ya chanjo kwa mifugo kwa upande wa ng'ombe Sh. 500, mbuzi na kondoo Sh. 300 na kuku Sh. 100, itakuwa sawa na bure," aliongeza Dk. Kijaji.

Aliwataka viongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Manispaa na Jiji kutoa ushirikiano kwenye kampeni hiyo ya chanjo ili kufanikisha malengo ya serikali kutokomeza magonjwa hayo.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Profesa Riziki Shemdoe, alisema chanjo hiyo itahusisha wataalam na wafugaji na kuwataka kutoa ushirikiano.



# Wataalamu TMA, miamba sasa kuchunguza radi Ludewa

## -Ni kutokana na kuua watu na mifugo mara kwa mara

**Na Elizabeth John,**
LUDEWA

WATAALAMU wa Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) kwa kushirikiana na wa miamba wanatarajia kufanya tafiti na kudhibiti radi kuendelea kusababisha vifo vya watu na wanyama wilayani hapa Mkoa wa Njombe.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Olivanus Thomas, katika Kijiji cha Kiwe Kata ya Mawengi wakati wa maziko ya watu watatu waliokufa kwa kupigwa na radi Sixbeth Haule (58), Emilian Mlelwa (55) na Lufina Ngailo (52).

Watu hao, walikumbwa na mkasa huo Desemba 15, mwaka huu majira ya saa 11 jioni katika Kijiji cha Kiwe, wakati watu hao wakiwa wamesimama nyumbani kwa Ngailo.

Thomas, alisema wiki mbili zilizopita watu wengine wanne walikufa kwa kupigwa radi, watatu wakiwa wa familia moja.

"Serikali tumeanza kufanya mawasiliano na Mamlaka ya Hali ya Hewa pamoja na wataalamu wa miamba ili waweze kuja kufanya tafiti na tujue namna gani tunaweza kudhibiti radi hii," alisema.

**"Serikali tumeanza kufanya mawasiliano na Mamlaka ya Hali ya Hewa pamoja na wataalamu wa miamba ili waweze kuja kufanya tafiti na tujue namna gani tunaweza kudhibiti radi hii," alisema.**

Alisema radi ni suala la hali ya hewa na kwa upande wa ardhi inafuata maeneo yenye miamba.

"Mtaalamu mmoja alinieleza watu wengi wanasema mvua ilikuwa kidogo ndio radi ikatokea, kwanini inapofika mwezi wa pili au watatu mvua zinakuwa nyingi hakuna radi. Radi wakati wote ni umeme ambao unatokana na mawingu," alisema.

Aliwataka wakazi wa wilaya hiyo kuachana na imani potofu kwa kuhusisha vifo vinavyotokana na radi na mambo mengine badala yake wanapaswa kutambua kuwa ni mipango ya Mungu.

Akitoa taarifa kuhusu vifo vya watu hao, pamoja na mambo mengine, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga, alitoa tahadhari kwa wananchi kuacha kukaa kwenye maeneo ambayo yana mvutano na radi ili kuepuka vifo vya aina hiyo.

Banga, alisema wataendelea kutoa elimu kupitia wakaguzi wa kata kuhimiza wananchi kuweka vikinga radi kwenye nyumba zao.




Katibu wa Sekreterieti ya Kamati Kuu ya CHADEMA, Julias Mwita, akimkabidhi fomu Dorcas Francis kwa ajili ya kuwania nafasi ya ujumbe wa kamati kuu, katika ofisi za makao makuu ya chama hicho, Mikocheni Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TASAF yaondoa chanjo kwenye turubai

**Na Faustine Feliciane**

UJENZI wa jengo la kutolea huduma ya mama na mtoto uliofanywa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Kituo cha Afya cha Makole jijini Dodoma umeondoa adha ya kupata chanjo kwenye turubai.

Kabla ya ujenzi wa jengo hilo, wakazi wa Kata ya Makole na maeneo ya jirani ya Swaswa na Ipagala walikuwa wakipatiwa huduma ikiwamo chanjo kwenye mazingira yasiyo rafiki.

Akizungumza kuhusu ujenzi wa jengo hilo uliofanywa na TASAF , Mtendaji wa Kata hiyo, Suzan Yohana, alisema wakazi hao walikuwa wanapata adha kwa kunyeshewa mvua wakati wa masika na vumbi kiangazi na kukosa hewa safi kwa kuwa eneo lilikuwa limefungwa turubai kwa ufinyu.

"Imekuwa faida kwetu na tunawashukuru TASAF kwa kujenga jengo hili ambalo sasa limesaidia huduma kutolewa katika mazingira bora zaidi, TASAF wamekuwa wadau wazuri sana katika kuboresha huduma hizi za mama na mtoto," alisema Yohana.

Kaimu Muuguzi Mfawidhi wa Kituo hicho, Joyce Kimario, alisema idadi ya watu waliokuwa wakifika kupata huduma katika kituo hicho ilikuwa ndogo ikilinganishwa na sasa baada ya mfuko huo kuwajengea jengo hilo.

Mwanakamati anayeshughulikia mpango wa walengwa wa TASAF ngazi ya mtaa, Neema Tandi alisema: "Wakati kukiwa na turubai kuna muda huduma zilikuwa zinasimama kutokana na upepo na mvua kusababisha kuanguka.

# Wafanyabiashara mji wa Njombe waamriwa kurejea sokoni

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BAADHI ya wafanyabiashara wa Halmashauri ya Mji wa Njombe wametakiwa kuondoka kwa hiyari kwenye maeneo yasiyo rasmi ili kukwepa mkono wa sheria.

Amri hiyo ilitolewa juzi na Mtendaji wa Kata ya Njombe Mjini, Enocy Lupimo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Njombe Kuruthum Sadick wakati wa kampeni ya kufanya usafi katika Mtaa wa Buguruni.

Lupimo, alisema halmashauri hiyo imeagiza wafanyabiashara waliotoa bidhaa sokoni na kupeleka barabarani kuondoa kabla hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao.

"Lazima tujizatiti katika suala la usafi na ninapeleka salamu stendi ya zamani, mkurugenzi ametoa vizimba soko kuu watu wanatoka wanaenda kupanga bidhaa stendi, kama una shangazi anauza pale vitumbua waambieni watoke kwa hiyari," alisema.

Akizungumzia kuhusu usafi, alisema kampeni hiyo ni mwendelezo ili kutunza mazingira katika mitaa yote tisa ya kata hiyo na kudhibiti kuibuka kwa magonjwa ya milipuko.

Mratibu wa Chanjo Halmashauri hiyo, kwa niaba ya Ofisa Afya, Simon Ngassa, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari kwa kufanya usafi ili kujikinga na maradhi yanayotokana na uchafu.

"Tuchukue tahadhari zote za usafi lakini pia watoto wapate chakula cha moto na wale wafanyabiashara yaani mama lishe wanaotuhudumia hakikisheni kwenye mgahawa mna maji safi ya kunawa na sabuni ya maji sio kipande, pia muwaeleze wale wanaofanya biashara barabarani warudi sokoni," alisema Ngassa.

Polisi Kata wa Njombe Mjini, Frolida Kietta aliwataka wananchi kuchukua tahadhari kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka kwa kuongeza ulinzi kwa watoto ili kuepuka ukatili wa kijinsia.

# Marekani yaipatia Tanzania vyandarua milioni 20

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya vyandarua milioni 20 vitasambazwa nchini na kugawiwa kwa wananchi milioni 35 kujikinga na ugonjwa wa malaria.

Hatua hiyo inafuatia Shirika la Misaada la Kimataifa Marekani (USAID) kukamilisha Mradi wa Kudhibiti Vidudu vya Malaria wa Rais wa Taifa hilo (PMI).

Vyandarua hivyo vilivyowekwa dawa za kuua mbu wanaosambaza malaria vitatolewa katika mradi huo wa miaka minne kwa matumizi ya watu hao zaidi milioni 35 wa Tanzania Bara na Visiwani.

Taarifa kwa umma iliyotolewa hivi karibuni na Mkurugenzi wa Misheni ya USAID, Craig Hart ilisema kuwa wamekwisha kusambaza baadhi ya vyandarua kupitia kampeni katika shule na vituo vya afya kwa makundi hatarishi ya watoto wachanga na wajawazito.

"Ushirikiano wa Marekani na Tanzania unachukua zaidi ya miongo sita na tangu mwaka 2006, PMI imewekeza zaidi ya Dola milioni 747 kukabiliana na malaria nchini Tanzania.

"Tunajivunia mafanikio ya mradi wa PMI. Ingawa mradi huu mahususi umekamilika, dhamira yetu ya kushirikiana na watu wa Tanzania kukabiliana na ugonjwa wa malaria na changamoto nyingine za afya ya jamii bado haijayumba," alisema Alisema kuanzia mwaka 2020 hadi 2024, mradi wa Dola milioni 43, ukiongozwa na Kituo cha Johns Hopkins cha Mipango ya Mawasiliano kwa ushirikiano na Tropical Health LLP na Viamo PBC, uliunga mkono juhudi za kulinda asilimia 90 ya watu walio katika hatari.

**"Ushirikiano wa Marekani na Tanzania unachukua zaidi ya miongo sita na tangu mwaka 2006, PMI imewekeza zaidi ya Dola milioni 747 kukabiliana na malaria nchini Tanzania.**

Alisema juhudi hizo zililenga mikoa 14 yenye maambukizi makubwa ya malaria Tanzania Bara na mitano ya Zanzibar, ikiwa ni asilimia 57 ya watu wote wa nchini.

Mshauri wa Mpango wa PMI nchini, Naomi Serbantez alisema kwa kukuza utaalamu wa ndani na kutumia maarifa yanayotokana na takwimu, mradi huo umeweka msingi wa maendeleo endelevu kutokomeza malaria nchini.

Alisema mafanikio muhimu yalijumuisha kuimarisha uwezo wa mashirika ya usambazaji wa vifaa vya matibabu nchini kusimamia usambazaji wa vyandarua kwa uhuru, kuboresha vifaa vya usafirishaji kupitia zana za kisasa na mifumo ya kufuatilia kwa wakati halisi na kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa juhudi za kuzuia malaria.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar , Othman Masoud Othman (kulia) akimsikiliza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhandisi, Hamad Yusuf Masauni alipokwenda kujitambulisha kwake hivi karibuni. **PICHA: ROBERT HOKORORO**

# TCRA yawanoa wazee kukabili utapeli

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MENEJA wa Ofisi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Zanzibar, Esuvatie-Aisa Masinga, amesema wataendelea kutoa mafunzo kwa makundi ili kukabiliana na tatizo la utapeli nchini.

Akizungumza wakati wa mafunzo kwa wazee wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja katika kampeni yao ya 'Ni rahisi sana' inayotolewa na TCRA mjini hapa, Masinga, alisema kwa sasa teknolojia inakuwa nchini na mambo ya usalama mtandaoni huku waathirika wakuu wakiwa ni wazee.

Alisema mafunzo hayo yatawasaidia kujilinda na utapeli huo na kuwasisitiza wanapopata viashiria vya vitendo hivyo, watoe taarifa kwa mamlaka hiyo na polisi.

Hivyo, aliwataka kuendelea kujilinda na kukataa kumpa mtu yeyote namba ya siri ya siku yake ili kuepuka kutapeliwa.

Masinga, alisema kuanzia Juni hadi Septemba mwaka huu, katika Mkoa wa Mjini Magharibi laini zilizosajiliwa ni 518,053 na majaribio ya ulagai ni 122.

Mkuu wa Divisheni Pensheni ya Jamii na Maendeleo ya Wazee Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee, Bikame Sheha Ussi, alisema mafunzo hayo yamewapa faraja kwa kuzingatia mazingira ya sasa ya kuwapo kwa utapeli kwa wananchi.

Ussi, alisema wazee wakitapeliwa na watasababishiwa matatizo mbalimbali ikiwemo msongo wa mawazo na kupelekea kufa.

# Zanzibar kuendelea kukuza utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Utalii wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Dk. Abdulla Mohammed Juma amesema lengo la kuanzishwa matamasha na mashindano ya mbio za marathoni ya kimataifa ni kukuza utalii visiwani hapa.

Juma aliyasema hayo wakati akizungumza na waadishi wa habari kuhusu mbio hizo kwa mwaka huu yanayotarajiwa kufanyika Desemba 28, mwaka huu visiwani hapa.

Alisema juhudi hizo zinalenga kuitangaza Zanzibar kama kivutio cha pekee cha utalii duniani.

Alisema mbio hizo zitahamasisha wageni wa kimataifa na wa ndani ya nchi kutembelea visiwa hivyo na kuliongezea taifa mapato.

Mkurugenzi huyo, alisema matukio kama hayo husaidia kuongeza idadi ya watalii na kuchangia kukuza uchumi wa Zanzibar kupitia huduma za hoteli, usafiri na sekta nyingine za utalii.

Juma, alisema mashindano hayo yanaimarisha mshikamano katika jamii na kuibua vipaji vya michezo miongoni mwa wakazi wa visiwani hapa.

"Hatua hii ni moja ya mikakati muhimu ya kutangaza vivutio vya Zanzibar kama fukwe zake, utamaduni wake wa kipekee, na historia yake tajiri," alisema.

Alisema kuwa katika jambo hilo mkakati mkubwa ni kuongeza bidhaa za kitalii za Zanzibar kwa kutoa msukumo upande wa utalii wa historia na mambo ya kale ,utalii wa michezo ,utalii wa vyakula na utalii wa mikutano ili kuongeza siku za wageni kukaa visiwani Zanzibar.

Alisema kuwa ukweli usio fichika kuwa sekta ya utalii ni sekta mtambuka ambayo inategemea na kutegemewa na sekta nyingine tofauti.

Mwakilishi wa mbio hizo za Touch Toad China Marathon, Zeng Peng alisema wanaunga mkono jitihada za serikali kukuza utalii ili kuongeza idadi ya watalii kuitembelea Zanzibar.



Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Zainab Katimba akizungumza na wananchi katika Shule ya Msingi Madizini wilayani Mvomero Mkoani Morogoro kwenye hafla ya kukabidhi bendera ya kijani kutoka taasisi ya elimu na mazingira duniani FEE kwa shule 26 za halmashauri nne za wilaya za Morogoro, Kilosa na Mvomero mkoani humo na wilaya ya Mufindi mkoani Iringa. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Ajifungua watoto wanne, apata tatizo la upumuaji

**Na Titus Mwombeki, BUKOBA**

MKAZI wa Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, Raina Mathew (34), amejifungua watoto wanne katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera Bukoba (BRRH) na kupewa rufani kwenda Hospitali ya Rufani Kanda Bugando kwa ajili ya uangalizi zaidi.

Mama huyo ambaye pia ni mke wa mwandishi wa habari mkoani hapa, Benson Eustace, alijifungua pacha hao wiki mbili zilizopita kisha kupewa rufani kutokana na tatizo la upumuaji na sasa anaendelea na kliniki baada ya kuruhusiwa.

Daktari Bingwa wa Watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera, Dk. Mike Mabimbi alisema mama huyo baada ya kujifungua, alipatiwa rufani kutokana na tatizo la kupumua alilolipata wakati wa kujifungua.

Alisema watoto hao wanaendelea kupewa uangalizi kutokana na kuzaliwa chini ya uzito wa kilo 1.5 badala ya kilo 2.5 zinazohitajika.

"Kwa sasa maendeleo yao ni mazuri. Wameanza kuongezeka uzito na wanapata huduma stahiki kama watoto wengine waliopo hospitalini hapa. Angalizo letu ni kwamba pindi watakaporuhusiwa kwenda nyumbani wasianze kutembelewa na watu kuwaangalia mpaka pale tutakapotoa ruhusa," alisema Dk. Mabimbi.

Alisema kitendo cha kuwepo kwa mwingiliano wa watu pindi wanaporudi nyumbani kinasababisha kuongezeka kwa athari na maradhi kwa watoto hao.

Ofisa Lishe, Victoria Ngatunga, alisisitiza umuhimu wa lishe yenye virutubisho vingi kwa kina mama wanaonyonyesha, akiwashauri kula mara kwa mara, huku akizingatia vyakula vya kimiminika ili kuchochea uzalishaji mwingi wa maziwa.

Akizungumza na Nipashe, baba wa watoto hao, Eustace, alisema mke wake alijifungua watoto wanne, wawili wakike na wawili wa kiume na mpaka sasa wanaendelea kupata huduma hospitalini hapo wakisubiri hali zao kutengamaa.

Eustace alisema kliniki hiyo ni kwa ajili ya uangalizi ambako alirudi juzi na kufanyiwa vipimo, kisha kuruhusiwa na kutakiwa kurudi tena Januari 20, mwakani.

Alisema watoto bado wanaendelea kupatiwa huduma na kuwa tayari wametoka kwenye hatua ya uatamizi (incubation) na sasa wameanza kuwakumbatia ambako walihitajika ndugu kwa ajili ya kusaidia huduma hiyo.

"Kikubwa ambacho tumeambiwa na madaktari ni kuhakikisha watoto wanapata maziwa na kwa sasa wanaendelea vizuri na mambo mengine yapo ndani ya uwezo wa madaktari," alisema.

Mkuu wa Mkoa Kagera, Fatma Mwassa akizungumza alipotembelea watoto hao kuwajulia hali, aliwapongeza madaktari na wauguzi wa hospitali hiyo kwa jinsi wanavyoendelea kuwapa huduma bora kuwanusuru pacha hao na kuhakikisha wanarejea katika hali yao ya kawaida.

Alisema watoto hao wanaoendelea kupatiwa huduma na uangalizi hopitalini hapo na wataalamu mbalimbali mpaka pale watakapokuwa katika hali yao ya kawaida na mama yao kuwa tayari kuwahudumia.

# PPP kuimarisha utekelezaji miradi mikubwa

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WATAALAM wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi nchini wameagizwa kuhakikisha miradi yote mikubwa yenye mvuto wa kibiashara inatekelezwa kwa njia ya ubia baina ya pande hizo (PPP) ili kuipunguzia serikali mzigo wa gharama.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Jenifa Omolo, alisema hayo jana kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara, Dk. Natu Elmaamry Mwamba, wakati akifungua kikao cha kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tanzania kuhusu PPP.

Alisema utekelezaji wa miradi kupitia PPP ni sehemu ya kujenga uchumi imara na ni suala ambalo linatekelezwa na nchi nyingi duniani.

"Msiogope, hata nchi zilizoendelea zinateleza miradi yao kupitia PPP, ukiangalia madaraja na majengo mbalimbali wameyatekeleza kupitia PPP. Sekta binafsi wakipewa nafasi wanafanya vizuri", alibainisha.

Omolo aliwaagiza wataalam hao kukuza uelewa wa dhana ya PPP kwa wadau mbalimbali kwa kuwa bado kuna changamoto ya uelewa kuhusu suala hilo na faida zake.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Rashid Ali Salim, aliwaagiza wataalam hao kuhakikisha wanayafanyia kazi yale yote waliyokubaliana katika kikao hicho hususani kuwa na mkakati wa pamoja wa kuuza fursa na kuibua miradi ya PPP.

Kaimu Kamishna wa PPP, Wizara ya Fedha, Bashiru Taratibu, alisema katika kikao hicho kuna masuala mbalimbali wameazimia kuyatekeleza ikiwemo maboresho ya Sheria ili kurahisisha shughuli za PPP nchini hususani katika kutekeleza miradi ya pamoja kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.

"Tumejadili kuhusu miradi ya pamoja ambayo Sekta Binafsi inaweza kutekeleza kama mradi wa Daraja la Dar es Salaam hadi Zanzibar lakini kila sehemu wana sheria yao ya PPP, kwa hiyo tumekaa kuona namna bora ya kutekeleza suala hilo iwapo mwekezaji atajitokeza", alisema.

Alisema Tanzania inahitaji kuwa na sera au sheria ya PPP inayoelezea utekelezaji wa miradi ya pamoja kati ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kuwa suala kama hilo limeshajitokeza katika nchi za Afrika Mashariki na kuna miradi ambayo inaunganisha nchi moja na nyingine na kwa sasa tayari kumeshaandaliwa Sera ya PPP ya Afrika Mashariki.

Kamishna wa Kituo cha Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPPC), David Kafulila, alisema katika kikao hicho wamejadiliana mambo mbalimbali ya kurahisisha ubia nchini ili kuipunguzia mzigo serikali wa kugharamia miradi ya maendeleo ambayo inaweza kugharamiwa kupitia PPP.

Alisema Tanzania kwa sasa inafanya vizuri katika eneo la PPP na kwamba kwa Tanzania Bara, kuna takribani miradi 74 ambayo iko katika hatua za mwisho kuanza kutekelezwa na Zanzibar kuna takribani miradi 13.


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDULI RAMADHANI MUSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 881 DPT** aina ya **TOYOTA COASTER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/28140/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ASHURA MOHAMEDI HAMISI** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE 241526** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 18/11/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIG/280043/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AUGUSTINO JOHN MAGESSA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA BLUE CARD YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 653 EJY,** AINA YA GARI NI TOYOTA IST-PEARL , KWA YOYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.

TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MBE/MBE/41860/2024.**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 31737 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late: VERONICA ANDREA BANZI**

**By 1. FARID JIRANI MAGOMA**
**2. ..........................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 24 day of 1.2025

Dated at MOROGORO this 18 day of 12.2024

..............................
**RESIDENT MAGISTRATE**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE DISTRICT COURT P.O.Box 660, Morogoro

## KUPOTEA KWA VYETI



**JOEL GABRIEL JUMA,** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE INDEX NAMBA **S3692-0086** MWAKA 2015 KINKATI SECONDARY SCHOOL, KIDATO CHA SITA INDEX NAMBA **S0554-0638** MWAKA 2018 NGUDU SECONDARY SCHOOL NA CHETI CHA UALIMU NAMBA **E0502/0096** MWAKA 2020 KLERRUU TEACHER'S COLLEGE. RIPOTI YA POLISI IMETOLEWA **PHQ/MWA/NYA/32025/2024, PHQ/SIM/MEA/3556/2024, PHQ/SIM/MEA/3558/2024.** YEYOTE ATAKAYEVIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU NAYE.

# Serikali mpya Syria yaomba kuondolewa vikwazo kiuchumi

**DAMASCUS, Syria**

KIONGOZI wa serikali ya mpito nchini Syria, Ahmed al-Sharaa, amesema nchi hiyo imechoshwa na vita na sasa sio tishio kwa majirani na nchi za Magharibi.

Akizungumza na BBC mjini Damascus, Al-Sharaa aliomba vikwazo dhidi ya Syria viondolewe.

"Sasa, baada ya yote yaliyotokea, vikwazo lazima viondolewe kwa sababu vililengwa kwa utawala wa zamani. Mwathiriwa na mdhalimu hawapaswi kutendewa sawa," alisema.

Sharaa aliongoza mashambulizi yaliyoangusha utawala wa Bashar al-Assad chini ya wiki mbili zilizopita. Yeye ni kiongozi wa Hayat Tahrir al-Sham (HTS), kundi kubwa katika muungano wa waasi, na hapo awali alijulikana kwa jina la Abu Mohammed al-Jolani.

Alisema HTS inapaswa kuondolewa kwenye orodha ya makundi yanayotambulika kama mashirika ya kigaidi.

HTS imetajwa na Umoja wa Mataifa, Marekani, EU na Uingereza, kuwa miongoni mwa makundi ya kigaidi kutokana na kugawanyika kwa kundi la al-Qaeda mwaka 2016.

Sharaa alisema HTS sio kundi la kigaidi kwani hawakuwalenga raia au maeneo ya kiraia wakati wa mapigano.

Alikanusha kuwa alitaka kubadilisha Syria kuwa kama Afghanistan.

Aidha, Sharaa alisema nchi hizo ni tofauti na zenye mila tofauti.

Aliongeza kuwa anaamini katika elimu kwa wanawake.

Hata hivyo, raia wengi wa Syria bado hawamwamini.

Mtazamo wa serikali mpya katika miezi michache ijayo utaonesha aina gani nchi hiyo inavyokwenda.

Wakati huo huo, Russia inaondoa vifaa vyake vya kijeshi nchini Syria, ikiashiria maandalizi ya kujiondoa katika nchi hiyo.

Picha za satelaiti zinaonesha mkusanyiko wa magari ya kijeshi katika bandari inayodhibitiwa na Russia ambayo ni kambi ya wanajeshi wa anga iliyoko magharibi mwa Syria.

Ndege za usafiri pia zimeonekana kuwasili na kuondoka nchini humo katika siku za hivi karibuni.

BBC imeona video zinazoonesha safu za malori ya kijeshi za Russia zikielekea kaskazini kwenye vituo vya kijeshi.

Taasisi ya Utafiti wa Vita ilieleza inaonesha maandalizi ya kupunguzwa au kuondoka kabisa kwa vikosi vya Russia nchini humo.

Taasisi hiyo yenye makao yake makuu mjini Washington iliongeza kuwa, kuhamisha magari ya kijeshi katika kambi zake huenda ikawa hatua ya tahadhari wakati Russia ikijadiliana na serikali mpya.

Wiki iliyopita meli za kivita za Russia ziliondoka kwenye bandari ya Tartous, huku wachambuzi wakieleza kwamba zilikuwa zikiwekwa katika maji ya kimataifa kwa wakati huo.

Hata hivyo, meli hizo hazijarudi lakini zaidi ya magari 100 ya kijeshi yamewasili katika kambi hiyo siku za hivi karibuni kwa mujibu wa picha za satelaiti zinavyoonyesha.

***BBC***



Wafanyakazi wakijaribu kuzima moto baada ya jeshi la Israel kushambulia kituo cha umeme nchini Yemen jana. **PICHA: REUTERS**

# Israel yafanya shambulizi Yemen

**SANAA, Yemen**

Israel imefanya mashambulizi ya anga katika ngome za waasi wa Kihouthi nchini Yemen na kuua watu tisa.

Hatua hiyo inatokana na wanamgambo hao wa Kihouthi, kushambulia kwa kombora mji wa Tel Aviv na kusababisha shule moja kuteketea.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Israel, kwamba kombora hilo lilitunguliwa na mabaki yake yalianguka karibu na mji huo na kuharibu vibaya shule moja.

Hata hivyo msemaji wa jeshi la Israel alisema hakuna kifo kilichotokea kutokana na tukio hilo,.

Waasi wa Kihouthi wanafanya mashambulizi hayo kuwaunga mkono Wapalestina katika Ukanda wa Gaza.

Mashambulizi ya Israel yaliyofanyika jana yanatishia kutanuka kwa machafuko kati ya Israel na Wahouthi ambao wanaoungwa mkono na Iran.

Jeshi la Israel lilisema limefanya mashambulizi mawili ya angani katika operesheni iliyopangwa awali na kuanza jana na kuhusisha ndege za kivita 14.

Aidha, jeshi hilo lilieleza shambulizi la kwanza lililenga miundombinu ya Wahouthi katika bandari za Hodeida, Salif na kituo cha mafuta cha Ras Isa katika Bahari ya Shamu.

Katika mashambulizi ya pili, ndege za kivita za Israel zililenga miundo mbinu ya nishati iliyoko mji mkuu wa Sanaa.

Shirika la Habari la al-Masirah linalodhibitiwa na Wahouthi lilisema baadhi ya mashambulizi yalipiga vituo vya umeme vilivypo katika mji wa Sanaa.

***DW.***

# Macron atembelea Mayotte

**PARIS, Ufaransa**

RAIS wa Ufaransa Emmanuel Macron, ametembelea kisiwa cha Mayotte kutathmini uharibifu uliosababishwa na kimbunga Chido.

Kimbunga hicho kimepiga visiwa vya Bahari ya Hindi na Msumbuji na kusababisha vifo, uharibifu wa mali na miundombinu mbalimbali.

Ziara yake katika kisiwa hicho kinachotawaliwa na Ufaransa inakuja baada ya juzi usiku serikali kutangaza hatua za dharula kutokana na janga hilo la asili katika kisiwa hicho cha Mayotte ili kuwezesha usimamizi mzuri wa kukabiliana na janga.

Hata hivyo, maofisa wameonya kwamba idadi ya vifo kutokana na kimbunga hicho kibaya zaidi kutokea katika historia ya eneo hilo, vinaweza kufikia mamia au pengine maelfu wakati waokoaji wapo katika kazi ya kuondoa vifusi kwenye mitaa ya mabanda ili kutafuta manusura.

Idadi ya awali kutoka kwa wizara ya mambo ya ndani ya Ufaransa, inaonyesha kuwa watu 31 wamethibitishwa kufa na wengine 1820 wamejeruhiwa.

Wakati huo huo, idadi ya vifo vilivyotokana na kimbunga Chido nchini Msumbiji imeongezeka na kufikia watu 45.

Takwimu iliyotolewa na taasisi ya kitaifa ya kudhibiti majanga nchini humo, ilisema awali ilirekodiwa watu 34 walifariki Dunia baada ya kimbunga hicho kuupiga mkoa wa kaskazini wa Cabo Delgado Jumapili.

Katika taarifa yake ya ilisema watu 38 wamepoteza maisha mkoa wa Cabo Delgado, wanne Nampula, na watatu katika eneo la Niassa, ambalo liko ndani ya taifa hilo.

Takriban nyumba 24,000 zimeharibiwa kabisa na nyingine 12,300 zikiachwa na athari zinazoweza kufanyiwa marekebisho.

***DW***

# Eco Fashion Show kubeba wabunifu

**Na Faustine Feliciane**

ONYESHO la mitindo lililopewa jina la 'Eco Fashion Show' linatajwa kufundisha jamii ubunifu kwa kutumia rasilimali mbalimbali zilizopo nchini ambazo zina ubora, imeelezwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Tarafa wa Kariakoo jijini, Dar es Salaam, Adrian Kishe, alisema onyesho hilo limekuwa na tija kwa wabunifu na wanamitindo na lina lengo kujifunza namna kufanya kazi za ubunifu zenye kuleta tija.

Kishe alisema serikali itaendelea kuunga mkono miradi mbalimbali inayobuniwa kama hiyo ya mitindo ambayo inaleta tija si tu kwa wabunifu bali kwa jamii nzima ya Watanzania.

Alitoa wito kwa wabunifu na wanamitindo kuendelea kutumia majukwaa yao ya 'Fashion Show' ili kuhamasisha matumizi ya bidhaa rafiki kwa mazingira na kuzalisha bidhaa zinazoheshimu utamaduni wa taifa.

''Za Kwetu Eco Fashion Show sio tu maonyesho ya mitindo bali ni jukwaa inaloonyesha uzalendo na uwajibikaji wa kijamii, tumeshuhudia vipaji mbalimbali vya wabunifu wetu wakitumia malighafi za asili na za kirafiki kwa mazingira.

Hii ni ishara Tanzania ina hazina kubwa ya ubunifu ambayo inaweza kufanikisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii," alisema Kishe.

Aliongeza ubunifu wa kijani ni kichocheo muhimu cha maendeleo endelevu ambapo kupitia mitindo wanaweza kufanikisha kupunguza athari mbaya kwa mazingira.

Awali akimkaribisha mgeni rasmi, Mkurugenzi wa Shirika la Ladies Joint Forum (LJF), ambao ndio waratibu wa onyesho hilo la mitindo, Fransisca Mboya, alisema onyesho hilo limeandaliwa kwa dhamira ya kukuza ubunifu, kulinda mazingira na kuimarisha uchumi wa kijani kupitia sekta ya mitindo.

Mboya alisema LJF kama waandaaji wakuu wa onyesho hilo wanaamini wanawake ni nguzo muhimu katika juhudi za maendeleo endelevu.

"Kupitia jukwaa hii tunalenga kutoa nafasi kwa wabunifu hususan wanawake kuonyesha vipaji vyao na kuhamasisha matumizi ya malighafi za asili zinazojali mazingira.Onyesho hili ni matokeo ya kazi ya pamoja kati ya wabunifu,wadau wa mazingira na wanamitindo ambao wamejitolea kuleta mabadiliko chanya katika jamii," Mboya alisema.

Alisema kupitia ubunifu wa kijana jamii inaweza kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na kujenga mustakabali bora kwa kizazi kijacho.

# NAMUNGO, JKT TANZANIA VITA YA HESHIMA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

MBIO za kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara zinatarajia kuendelea tena kwa wenyeji Namungo FC kuwakaribisha JKT Tanzania katika mechi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani, Lindi.

Namungo watashuka katika mechi hiyo wakiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi wa ugenini wa mabao 3-2 dhidi ya KenGold ya Mbeya Jumapili iliyopita.

Kuelekea mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Namungo, Juma Mgunda, ameahidi timu yake itaendeleza wimbi la ushindi.

Mgunda amesema ushindi waliopata ugenini umewafanya vijana wake wawe na morali zaidi na hali ya kujiamini, hivyo anatarajia kupata ushindi mwingine leo watakaposhuka kwenye ardhi ya nyumbani.

"Ule ushindi tulioupata dhidi ya KenGold umetusaidia sana, umewafanya vijana wangu kupata morali na kuona kumbe wakipambana wanaweza kupata matokeo mazuri, kutokana kuruhusu mabao mawili hadi kurudisha yote na kufunga matatu si mchezo, lakini tulifanya hivyo.

Tunajua JKT Tanzania ni moja kati ya timu ngumu, hasa kwenye eneo lao la ulinzi, lakini sisi tumejipanga na watarajie mechi ngumu kutoka kwetu," alisema kocha huyo wa zamani wa Coastal Union na Simba.

Ofisa Habari wa JKT Tanzania, Masau Bwire, ametamba wako tayari kuwapa burudani ya kutosha mashabiki wa mkoa wa Lindi na vitongoji vyake, lakini pia akiwaonya Namungo wajiandae kupata fedheha mbele ya mashabiki wao.

"Tunawaomba mashabiki wa mkoa wa Lindi, waje Uwanja wa Majaliwa kuangalia soka safi linalotandazwa na JKT Tanzania, lakini nawaambia Namungo leo wataadhirika kwa kupata fedheha mbele ya mashabiki wao kwa sababu hatutawaacha salama, tumekuja kuchukua pointi tatu," alitamba Bwire.

Utakuwa ni mchezo wa 15 kwa Namungo, ikimaliza michezo yake ya mzunguko wa kwanza huku ikiwa nafasi ya 12 ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kabla ya mechi ya leo, JKT Tanzania ambayo itacheza mechi yake ya 14, ikiwa nafasi ya saba baada ya kujikusanyia pointi 19 kibindoni.

Azam FC ambayo pia imemaliza mechi zake za mzunguko wa kwanza inaongoza msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 33 ikifuatiwa na Simba yenye pointi 31 huku Singida Black Stars yenye pointi 30 ikifuatia.

KenGold ya Mbeya yenye pointi sita na imecheza mechi 15 inaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali.



Kocha wa Timu ya Watoto ya Kituo cha Michezo cha JMK Park, Dickson Haule, (kulia), akitoa maelekezo kwa watoto wanaofanya mazoezi ya kucheza mpira wa miguu kwenye viwanja vya kituo hicho jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Prisons yakanusha kumtimua Makata

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Prisons imesema bado, Mbwana Makata, ni kocha wa timu hiyo licha ya kupata matokeo mabaya katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazoendelea.

Mara baada ya kipigo cha mabao 2-0 katika mechi iliyochezwa Jumatatu iliyopita kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya, dhidi ya Singida Black Stars, kulizuka taarifa uongozi wa klabu hiyo umemtimua Makata.

Prisons inaendelea na maandalizi ya kuwafuata mabingwa watetezi, Yanga katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. Ofisa Mtendaji Mkuu wa Prisons, John Matei, aliliambia gazeti hili jana, taarifa hizo hazina ukweli wowote, badala yake bado kocha huyo anaendelea na majukumu huku akiwa amebakisha miezi saba kwenye mkataba wake.

"Mwalimu Makata bado tupo naye na tuna mkataba naye, amebakisha miezi saba, sijajua taarifa hii imetoka wapi. Mimi ndiyo Mtendaji Mkuu ninayeongea, kwa hiyo nasema jambo lenye uhakika, hivi ninavyokwambia ametuachia kazi ya kuratibu safari, na ameshatupa majina ya wachezaji ambao wataambatana kwenye hiyo safari kwenda Dar," alisema Matei.

Prisons haijashinda ushindi katika michezo minne mfululizo ya Ligi Kuu, tangu ilipopata ushindi mara ya mwisho, Novemba 3, mwaka huu kwa kuifunga KenGold bao 1-0.

Makata alijiunga na Prisons akitoka kuipandisha daraja hadi Ligi Kuu, Pamba Jiji ya Mwanza huku Wajelajela hao wakiwa wamemtimua aliyekuwa Kocha Mkuu, Fred Minziro, ambaye kwa sasa naye yuko Pamba.

## ZISIKUPITE

### GUEHI ATAKIWA CITY

KLABU ya Manchester City inavutiwa na beki wa Crystal Palace na England, Marc Guehi, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 akionekana kama anaweza kuwa sehemu ya marekebisho ya safu ya nyuma ya timu hiyo. ***(Football Insider)***

### MADRID YAMTAKA RASHFORD

ATELTICO Madrid wanaweza kumnunua kwa mkopo mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford, mwenye umri wa miaka 27, ambaye hachezeshwi katika kikosi cha kwanza, Old Trafford. ***(TBR Football)***

### RASGFORD ATAKIWA SAUDIA

KLABU za nchini Saudi Arabia pia zinavutiwa na mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford na zinaamini yeye ndiye mchezaji sahihi wa kuongeza hadhi katika ligi hiyo duniani. ***(Telegraph)***

### HALL KUTUA ARSENAL

ARSENAL inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Kiernan Dewsbury-Hall, mwenye umri wa miaka 26 katika dirisha la usajili la Januari. ***(Caught Offside)***

### ALMIRON SOKONI ENGLAND

KLABU za Crystal Palace, Leicester na Wolves zote zimeonyesha nia ya kumsajili fowadi wa Newcastle United na Timu ya Taifa ya Paraguay, Miguel Almiron, mwenye umri wa miaka 30 Januari. ***{Sun)***

### FERGUSON ANUKIA CITY

KLABU ya Manchester City inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Brighton na Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson, mwenye umri wa miaka 20. ***(GiveMeSport kupitia Caught Offside)***

### TRENT KITAELEWEKA

LIVERPOOL imempa beki wa kulia wa England, Trent Alexander-Arnold, mwenye umri wa miaka 26 ofa ya mkataba ulioboreshwa, lakini Real Madrid watazidisha juhudi zao za kumsaini kwa mkataba wa bila malipo msimu ujao wa joto na kukutana naye Januari. ***(Caught Offside)***

### SLOT AMKATAA FRIMPONG

LIVERPOOL haina uwezekano wa kumnunua mlinzi wa Bayer Leverkusen na Uholanzi, Jeremie Frimpong (24), ikiwa Trent Alexander-Arnold, ataondoka kwa sababu Kocha, Arne Slot, angependelea beki wa kulia wa jadi, ambaye ni bora katika safu ya nyuma, na haamini hiyo inamfaa Frimpong. ***(Florian Plettenberg/Sky Germany)***

### TIERNEY NJIA MOJA

MLINZI wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Scotland, Kieran Tierney, mwenye umri wa miaka 27, ataondoka Arsenal msimu wa joto baada ya klabu hiyo kuchagua kutomwongezea mkataba mpya. ***(Athletic, external)***

### POGBA ATAJWA MARSEILLE

MARSEILLE inafikiria kumnunua, Paul Pogba, mwenye umri wa miaka 31, ambaye anatafuta klabu mpya baada ya marufuku yake ya kutumia dawa za kusisimua misuli kupunguzwa. ***(Goal)***

### MENDES KUTUA UNITED

KLABU ya Manchester United inamtaka beki wa kushoto wa Ureno mwenye umri wa miaka 22, Nuno Mendes, ambaye mkataba wake wa sasa na Paris St-Germain unataka kurefushwa zaidi hadi mwaka 2026. ***(Florian Plettenberg/Sky Germany)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI AWEKA HISTORIA MADRID

●●●Ni baada ya kocha huyo kufikisha mataji 15 akiwa na vigogo hao...

**DOHA, Qatar**

CARLO Ancelotti amekuwa kocha mwenye mataji mengi zaidi katika historia ya Real Madrid, baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Pachuca katika mechi ya Fainali ya Kombe la Klabu bingwa ya Dunia ya FIFA na kumfanya afikishe mataji 15 ndani ya klabu hiyo.

Katika misimu miwili ya kuinoa Madrid, kati ya mwaka 2013 na 2015, na kutoka 2021, Ancelotti ameshinda mataji matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mawili ya LaLiga, Copa del Reys, Supercopas na UEFA Super Cup.

Rekodi ya awali ilikuwa ikishikiliwa na kocha maarufu wa Madrid, Miguel Muñoz, ambaye alitumia miaka 14 kuinoa Madrid kati ya mwaka 1960 na 1974, akishinda mataji mawili ya Ulaya, mataji tisa ya ligi, mawili ya Copa del Rey na Kombe la Mabara.

"Nina furaha sana ... ni mafanikio," alisema Ancelotti kuhusu ushindi dhidi ya Pachuca hapi juzi.

"Tulichukua udhibiti kidogo na kumaliza mchezo vizuri. Tuna tofauti hizo za ubora kila wakati, lakini pia tunapaswa kuonyesha mtazamo sahihi. Leo, mwisho, nilipenda."

Vinícius Júnior, ambaye alifunga pamoja na Mbappé na Rodrygo, alimsifu Ancelotti kwa mafanikio ya klabu hiyo.

"Hongera, anastahili, anatupa uhuru, ni kamili kwa ajili yetu," alisema Vinícius Jr.

"Anastahili. Ameshinda kila kitu. Anatuongoza," alisema Fede Valverde akiiambia Telecinco baada ya mechi.

HABARI MICHEZO

# Nunez, Elliott waibeba Liverpool

**LIVERPOOL, England**



MABINGWA watetezi wa Kombe la Carabao, Liverpool walitinga nusu fainali ya michuano hiyo baada ya kupata ushindi wa 2-1 dhidi ya Southampton katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja St Mary's juzi, shukrani kwa mabao ya Darwin Núñez na Harvey Elliott.

Hata hivyo, Kocha wa Liverpool, Arne Slot alishuhudia ushindi huo akiwa jukwaani akitumikia adhabu.

Nunez alifunga bao dakika ya 24, akipiga shuti baada ya mpira wa kati uliopigwa na beki, Jan Bednarek, kutemwa na golikipa, Alex McCarthy.

Elliott alifunga bao la pili kwa Liverpool dakika nane baadaye alipoachia shuti kali kutoka kwa Cody Gakpo.

Cameron Archer alirudisha bao moja kwa timu ya nyumbani dakika ya 59 kwa shuti kali kutoka ndani ya eneo la hatari.

"Tulikuja kwenye mchezo huu tukijua mazingira ambayo Southampton walikuwa wanapitia na tulijua watatoka kupigana na tulikuwa tayari kwa hilo," alisema Elliott akiiambia Sky Sports.

Mchezo huo ulikuwa kwa timu zilizo kwenye ncha tofauti za msimamo wa Ligi Kuu England, huku Liverpool wakiwa kileleni na Southampton wakiwa mkiani.

"Tunatakiwa kutetea kombe kwa sababu klabu ilitwaa msimu uliopita, hivyo tunataka kushindana katika kila ligi na hii ni moja wapo, hivyo tunafuraha kufika nusu fainali," alisema Slot.

# Acheampong mkataba mpya Chelsea

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea wamemwongezea beki wake wa kulia, Josh Acheampong, mkataba mpya wa miaka mitano ambao utamweka klabuni hapo hadi mwaka 2030.

Mchakato huo unahitimisha uvumi juu ya hatima ya beki huyo baada ya kukubaliana na mabosi wake kuboreshwa kwa mkataba wake.

Baada ya kucheza kwa dakika chache kwenye mechi ya Kombe la Carabao mwanzoni mwa msimu huu, kinda huyo aliwekwa kando kufuatia kukataa majadiliano ya mkataba mpya.

Vigogo Liverpool, Real Madrid and Bayern Munich walitajwa kuwania saini ya beki huyo kiraka ambaye mkataba wake wa sasa ungemalizika katikati ya msimu ujao

Lakini mazungumzo yenye tija ya kuongeza mkataba wa beki huyo yalifanyika katikati ya mwezi uliopita, ikashuhudiwa Acheampong akirejea kwenye mazoezi ya kikosi cha kwanza cha Chelsea.

Kinda huyo alikanyaga boli kwa dakika 90 akiwa sehemu ya kikosi kilichoibugiza Astana mabao 3-1 kwenye Ligi ya Europa Conference Alhamisi iliyopita.



# HAT-TRICK YA JESUS YAIPAISHA ARSENAL

**LONDON, Englabd**

GABRIEL Jesus alifunga 'hat trick' kipindi cha pili wakati Arsenal ilipotoka nyuma na kuifunga Crystal Palace mabao 3-2 na kutinga nusu fainali ya mashindano ya Kombe la Carabao mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Emirates juzi usiku.

Palace walijiweka mbele kwa bao la Jean-Philippe Mateta aliyempita kiurahisi Jakub Kiwior na katika dakika ya nne.

Lakini Arsenal walitawala zaidi kipindi cha pili na Jesus akasawazisha dakika ya 54 wakati Martin Odegaard alipocheza vizuri na kumpa pasi mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil ambaye alimfunga golikipa, Dean Henderson.

Jesus alifunga la pili katika dakika ya 73 kwa pasi ya Bukayo Saka na alikamilisha hat trick yake dakika nane baadaye alipokimbilia mpira kutoka kwa Ødegaard nyuma ya safu ya nyuma ya Palace kabla ya kumfunga Henderson.

"Nimefurahishwa sana na Jesus. Umekuwa muda mrefu kwake bila mabao," alisema Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, akiwaambia waandishi wa habari.

"Kufunga aina tatu za mabao na vitendo vingi ambavyo alihusika, ni jambo kubwa kwa timu ambayo tunaweza kumtegemea mchezaji mwenye ubora kama huu."

Mchezaji wa zamani wa Arsenal, Eddie Nketiah, aliifungia Palace bao moja dakika za lala salama aliporuka kwa kichwa na kumpita David Raya.

# MPANZU RASMI KUITUMIKIA MSIMBAZI LIGI BARA, CAF

**Na Adam Fungamwango**

WEKUNDU wa Msimbazi wametangaza rasmi winga, Elie Mpanzu, ataanza kuitumikia timu hiyo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba mkoani, Kagera baada ya kupata Hati ya Uhamisho wa Kimataifa (ITC).

Mpanzu ambaye alisajiliwa na Simba akiwa mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake na AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, pia tayari amepata leseni inayomruhusu kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema taratibu za vibali vya kazi vya Mpanzu vilikamilika juzi na sasa ataanza rasmi kuitumikia klabu yake mpya.

„Kuhusu Mpanzu mambo yake yote yameshakamilika, iliyobaki ni kocha (Fadlu Davids), mwenyewe tu, kama atamtumia, ila yuko tayari kuitumikia Simba, kwa maana hiyo wanachama na mashabiki wa Simba wawe tayari kumwona mchezaji huyo akiitumikia timu yao kwa mara ya kwanza,“ alisema Ahmed.

Maandalizi yanakwenda kufanyika huko huko Kagera, hatujafanya maandalizi yoyote baada ya mchezo wetu dhidi ya KenGold jana (juzi), tumeondoka leo (jana) na jioni ndiyo tutaanza mazoezi pamoja na kesho (leo).

Kwa misimu ya hivi karibuni, nadhani misimu mitatu hivi mfululizo, tumekuwa tukipata matokeo mabaya kwenye Uwanja wa Kaitaba, na tumekuwa tukipata shida dhidi ya Kagera Sugar, imekuwa ikitupotezea malengo yetu ya kuchukua ubingwa, safari hii hatukubali, tunataka kwenda kuchukua pointi tatu, tunafahamu haitakuwa rahisi kutokana na ubora wa mpinzani, lakini tumejipanga, haya ni mapambano,“ alisema meneja huyo.

Akizungumzia mchezo wa juzi dhidi ya KenGold, Fadlu, amewapongeza wachezaji wake kwa kupambana, kwa sababu wengi walikuwa na uchovu wa mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia, uliochezwa Jumapili iliyopita.

"Tuweke kumbukumbu sawa, wachezaji walifanya kazi kubwa sana katika mchezo wetu dhidi ya CS Sfaxien hasa kipindi cha pili kwa ajili ya kusaka bao la pili ambalo tulilipata mwishoni mwa mchezo, ndiyo maana leo (juzi), nimebadilisha kikosi kuwaweka wachezaji ambao miguu yao haijatumika sana kama Mzamiru Yassin, Kelvin Kijili na Velentino Nouma ambao wamekuwa kwenye uwango cha juu. Ratiba inaonyesha karibuni kila baada ya siku mbili tuna mechi, hivyo tunahitaji kila mchezaji awe tayari kutoa alichonacho na kuwapumzisha wengine,“ alisema Fadlu.

Omari Kapilima, Kocha Mkuu wa Ken-

# TFF yamfungia kigogo DRFA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Maadili ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imemfungia miaka mitano kujihusisha na mpira wa miguu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Dar es Salam (DRFA), Yusuph Kaiwanga.

Katika uamuzi wake, Kamati imesema baada ya kupitia ushahidi wa nyaraka na maelezo ya shahidi imejiridhisha pasi na shaka mlalamikiwa, Kaiwanga alitenda makosa kwa makusudi.

Kamati ilijiridhisha Kaiwanga hakutumia vyema mamlaka aliyopewa kisheria kusimamia uchaguzi wa Chama cha Mpira wa Miguu Wilaya ya Temeke (TEFA) na kuamua kuufuta.

Hatua yake ya kuufuta haikuwa sahihi kwa vile alishiriki mchakato mzima wa uchaguzi huo. Hivyo, Kamati ya Maadili imeamua matokeo ya uchaguzi wa TEFA yanabaki kama yalivyo.

"Mbali ya kifungo cha miaka mitano, Kamati pia imemtoza Kaiwanga kulipa faini ya Sh. milioni sita. Adhabu hizo zimetolewa chini ya kifungu cha 73 (4) na (5) cha Kanuni za Maadili za TFF, Toleo la 2021,“ ilisema sehemu ya taarifa hiyo ya TFF.

Wakati huo huo, Rais wa TFF, Wallace Karia, amempongeza, Salum Kulunge, kwa kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Geita (GEREFA).

Karia amewatakia uongozi mzuri Kulunge na Kamati ya Utendaji ya GEREFA.



Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa KenGold FC, Kazila katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Azam vitani rasmi ikiutaka ubingwa

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kukaa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam FC, imewapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kusema haijalishi kutokana na baadhi ya timu zinazoshiriki ligi hiyo bado hazijakamilisha mechi zao za mzunguko wa kwanza.

Azam FC inaongoza ligi ikiwa na pointi 33 ikifuatiwa na Singida Black Stars huku Simba yenye pointi 31 ikifuatia lakini imecheza michezo mitatu pungufu.

Ofisa Habari wa Azam FC, Hasheem Ibwe, amesema uongozi wa klabu hiyo umefurahishwa na viwango vya wachezaji wao na sasa wanawaza kupambana kuhakikisha wanatwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ibwe alisema haikuwa kazi rahisi kumaliza mechi 15 za mzunguko wa kwanza wakiwa na pointi 33 kibindoni kutokana na ushindani uliopo msimu huu.

"Tunawapongeza wachezaji wetu kwa kazi kubwa walioifanya mpaka kufikia hapa, kwa sababu msimu huu kuna ushindani mkubwa sana, nadhani kuliko misimu mingine iliyopita, kuna timu ambazo hazikuzungumzwa, lakini zimeonyesha upinzani mkubwa sana,“ alisema Ibwe.

## Gofu kumwenzi Lina Gymkhana Jumapili

**Na James Kandoya**

WAPENZI wa gofu nchini watakusanyika keshokutwa kwenye viwanja vya Gymkhana jijini, Dar es Salaam kushiriki mashindano maalumu ya kumwenzi mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya mchezo huo, Lina Nkya.

Lina anakumbukwa kwa mchango wake mkubwa katika mchezo huo, na urithi wake umejengwa kupitia ufanisi wa kipekee, juhudi zisizo na kifani na mapenzi kwa gofu ambayo yamehamasisha vizazi vingi.

Naye mchezaji wa gofu wa kulipwa kutoka mkoani wa Kilimanjaro, Isack Ayoub, alisema ni fursa, furaha kwake kushiriki katika mashindano hayo.

Ayoub alisema anapongeza uamuzi uliofanywa na familia ya Nkya kwa kushirikiana na Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU) kuenzi mchango wa nyota huyo.

"Kama mchezaji wa gofu wa kulipwa ni heshima kushiriki katika mashindano haya kumwenzi mchezaji mwenzetu wa zamani, tukio hili limeleta hamasa kubwa miongoni mwa washiriki. Sote tumejipanga vyema na kwa kufanya mazoezi ya ziada nina imani na nafasi yangu,“ alisema Habib.

Michezo
Ijumaa Desemba 20, 2024
Nipashe

## Ancelotti aweka historia Madrid

UKURASA 21






Mshambuliaji wa Yanga, Prince Dube (kushoto), akionesha ishara ya kumshukuru Mungu baada ya kufunga bao la kwanza msimu huu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mashujaa FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana. Kulia ni Pacome Zouzoua akimpongeza nyota huyo. Yanga ilishinda mabao 3-2. **PICHA: MTANDAO**

# DUBE AZINDUKA LIGI KUU

●●●Straika huyo Mzimbabwe apiga 'hat-trick' ya kwanza msimu huu...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA Prince Dube, raia wa Zimbabwe, ameweka rekodi ya kufunga mabao matatu maarufu 'hat-trick' na kuiongoza Yanga kupata ushindi wa mabao 3-2 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mashujaa FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana.

Mbali na kuwa ni 'hat-trick'ya kwanza msimu huu, lakini pia Dube ndio alikuwa anafungua akaunti yake ya mabao kwa sababu hakuwahi kupachika bao lolote kabla ya mechi hiyo.

Staika huyo ambaye tangu ajiunge na Yanga mwanzoni mwa msimu alikuwa na ukame wa mabao kiasi cha kuzua mijadala mbalimbali katika mitandao ya kijamii na vijiweni kwa mashabiki wa soka, alichaguliwa pia kuwa mchezaji bora katika mchezo huo.

Bao la kwanza katika mechi hiyo alilifunga dakika ya saba, akiunganisha krosi ya upendo iliyopigwa na kiungo mshambuliaji, Pacome Zouzoua, ilikuwa ni kazi iliyoanzia kwa Aziz Ki aliyenyang'anya mpira kutoka kwa wachezaji wa Mashujaa, akakimbia nao umbali mrefu kabla ya kuupiga kwenye wingi ya kulia kwa Pacome, ambaye aliurudisha ndani na kumkuta mfungaji.

Dakika ya 21, Dube alipachika bao la pili kwa kichwa, akimalizia kazi kubwa iliyofanywa na Pacome, kufuatia uzembe uliofanywa na mabeki wa Mashujaa.

Mpira huo ulileta kizaazaa langoni, awali Clement Mzize alikuwa afunge lakini ukambabatiza mchezaji wa timu pinzani, kabla ya kumkuta Dube aliyeusukumizia wavuni kwa kichwa.

Alitimiza 'hat-trick' yake dakika ya 52, akiunganisha kwa mara nyingine mpira kwa kichwa, krosi kutoka kwa Kibwana Shomari.

Hata hivyo haukuwa ushindi rahisi kwa Yanga, kwa sababu ililazimika kupambana kuhakikisha inaulinda kwa juhudi zote huku Mashujaa ikifanikiwa kupata bao dakika moja kabla ya mapumziko.

David Ulomi, alifunga bao hilo la kwanza la Mashujaa kwa shuti la mbali la kushtukiza, licha ya juhudi za kipa wa Yanga, Khomeini Aboubakar, kuruka kutaka kuokoa, lakini mpira ulimshinda na kujaa wavuni.

Wakati Yanga ikiongoza kwa mabao 3-1, dakika 10 baada ya kupata bao la tatu, Idriss Stambuli, aliipatia Mashujaa bao la pili ambalo lilifanana sana kama la kwanza kwa wageni hao.

Akiwa umbali wa mita takriban 35 hivi, aliachia shuti kali ambalo Khomeini alitaka kulidaka, lakini lilimshinda nguvu na kutinga wavuni.

Ushindi huo unaifanya Yanga kupanda hadi nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo ikifikisha pointi 30 sawa na Singida Black Stars, ikibebwa na uwiano mzuri wa mabao ya kufunga na kufungwa.

Mechi ilianza kwa kasi, ambapo dakika ya pili tu ya mchezo Yanga walikosa bao la wazi, wachezaji wake wawili, Stephane Aziz Ki, na Mzize walikosa bao, kila mmoja akitaka kuupachika wavuni bila mafanikio.

Krosi iliyopigwa na Yao Kouassi ilimkuta Aziz Ki ambaye aliunganisha shuti dhaifu lililowababatiza mabeki wa Mashujaa, ukamrudia Mzize ambaye alipiga mpira nje.

Dakika tatu baadaye, Duke Abuya nusura aipatie Yanga bao, kwani baada ya kupata pasi kutoka kwa Aziz Ki, alipiga shuti kali la mbali, lakini lilipaa juu.

Abdulnasir Mohamed Gamal, aliikosesha Mashujaa bao la wazi alipobaki yeye na Khomeini, lakini alichelewa kufanya maamuzi na kukutwa na mabeki wa Yanga akiwa bado hajaupiga mpira, wakaokoa.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena kesho kwa Kagera Sugar kuikaribisha Simba kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba mkoani, Kagera.

## Kamera mpya 200 Uwanja wa Mkapa kuwanasa wang'oaji viti

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema ufungaji kamera za kisasa za kufuatilia mienendo ya watu wote wanaoingia Uwanja wa Mkapa, mkoani Dar es Salaam, utaimarisha zaidi usalama na kuwanasa wote wanaovunja viti vya uwanja huo.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, akizungumza na waandishi wa habari jijini, Dar es Salaam jana, alisema maboresho yanayoendelea hivi sasa katika uwanja huo, yanajumuisha ufungaji kamera za kisasa 200 za kufuatilia mienendo ya watu wote wanaoingia uwanjani huko.

Alisema kamera hizo zikishafungwa, watakuwa na uwezo wa kufuatilia mienendo ya kila aliyemo uwanjani na nje ya uwanja, hivyo kuwanasa kwa urahisi wahalifu, wakiwamo wanaong'oa viti.

Hivi karibuni, viti 256 viliripotiwa kung'olewa na watazamaji muda mfupi baada ya filimbi ya mwisho ya mwamuzi wa mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika, ambayo wenyeji Simba walishinda mabao 2-1 dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia.

Katika hatua nyingine, Msigwa alisema Rais, Samia Suluhu Hassan ameeleza Wizara ya Fedha iandae fungu kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa soka wa kisasa mkoani Dodoma.

Alisema wameamua uwanja huo ujengwe kwa fedha za ndani kama wanavyofanya kwa Uwanja wa Samia, jijini Arusha.

Msigwa alisema, „ni kweli tuliahidiwa kujengewa uwanja Dodoma, lakini makubaliano yetu yalitufikisha mahali serikali ikasema tutumie njia nyingine ya kujenga huu uwanja.

"Sisi shida yetu ni uwanja, serikali imeamua kubadili njia ya ujenzi wa uwanja wetu. Na tutajenga kwa fedha zetu. Na utatumika kwa AFCON 2027 kwa sababu tuna SGR," alisema.

Msigwa pia alitangaza ujio wa Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Patrice Motsepe, anayezuru nchi kwa ajili ya kufuatilia maandalizi ya michuano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) yaliyopangwa kufanyika nchini Februari mwakani.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >